# KUISHI KWA IMANI
# KATIKA DUNIA ILIOVUNJIKA

Na Larry Chkoreff

Version 1.2 Desemba 2008
ISBN-978-0-9823060-0-0

Toleo la Kiswahili © 2010

Kimetafsiriwa na kuchapishwa na:
Cistern Materials Translation & Publishing Center, Nairobi, Kenya
Barua pepe: info@cisternmaterialscenter.com
www.cisternmaterialscenter.com

*Kuishi Kwa Imani Katika Dunia Iliyovunjika* kimechapishwa na International School of the Bible-ISOB, Marietta, GA USA
info@isob-bible.org
www.isob-bible.org

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Haki ya kumiliki © 2008 na Larry Chkoreff - Mwandishi

Kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Kinaweza kuchapishwa tena, iwapo tu kitachapishwa chote, kwa ajili ya kukisambaza bure (bila malipo). Hairuhusiwi kukibadili au kukihariri kwa njia yoyote ile. Kikichapishwa tena ni lazima kiwe na tangazo la miliki.

Vifungu vyote vya Biblia vimetolewa kutoka The Holy Bible in Kiswahili Bi UV052 BST/BSK © 2003 published by Bible Society of Kenya and Tanzania.

## YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................................................ 3

SURA YA 1 – MAELEZO YA JUMLA ................................. 6

SURA YA 2 – VIAMBATO VYA UVUMILIVU ………….. 18

SURA YA 3 – KUPIGA MBIO………………………………. 25

SURA YA 4 – KIAMBATO CHA UPENDO ………………. 34

SURA YA 5 - KIAMBATO CHA MATENDO………………. 45

SURA YA 6 - KIAMBATO CHA KUONGEA NENO……. 53

SURA YA 7 - VIAMBATO ZAIDI VYA PETRO……………. 62

SURA YA 8 – MFANO WA MPANZI ……………………….. 74

SURA YA 9 – KUSIKIA SAUTI YA MUNGU………………. 85

Reproduction, resale or internet posting prohibited

# Utangulizi
# Kuishi Kwa Imani
# Katika Ulimengu Uliyovunjika

Mungu alimpa Adamu mwaliko wa kushiriki katika Mti wa Uzima.

Mungu hakutarajia tuishi maisha haya kupitia nguvu zetu na uwezo wetu wenyewe. Anataka kuturejesha katika "maisha ya kawaida," mpango wake wa kwanza kwa mwanandamu. Katika Bustani la Adeni, alimpa Adamu chochote alichohitaji ili kuishi maisha tele. Mungu alimpa mamlaka juu ya ulimwengu na wanyama wote pamoja na mimea yote. Alimpa Adamu biashara ya kufanya pamoja na jamii yake, kuilima na kuitunza Bustani la Adeni.

Jukumu muhimu la Adamu lilikuwa kudumisha urafiki wake na Mungu, kusikiza Neno Lake kila siku, lililosimamiwa na Mti wa Uhai, kumtii na kutimiza amri za Mungu. Shetani aliwashawishi Adamu na Hawa waishi kulingana na hekima yao wenyewe. Aliwadanganya ya kwamba, kusikiliza Neno la Mungu kila siku halikuwa jambo la lazima. Pia aliwashawishi ya kwamba Mti wa kujua Mema na Mabaya, hekima yao, ilitosha bila Neno la Mungu.

Kurejea katika 'maisha ya kawaida' kunamaanisha kudumisha urafiki wa karibu sana na Yesu pamoja na Baba kupitia Roho Mtakatifu usiku na mchana. Tunaposikia Mungu akinena, imani inapandwa katika mioyo yetu kama mbegu, na ikidumishwa vilivyo, itazaa tunda ndani yetu. Tunda ni zaidi ya mambo yote ambayo tunahitaji katika maisha, uungu, na kwa ajili ya kueneza Ufalme wa Mungu hapa duniani.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

"Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye" (Waebrania 10:38). Andiko hili linamaanisha ya kwamba, wale ambao wamekuwa wenye haki kupitia kazi iliyokamilika ya Yesu Kristo kupitia kifo chake na kufufuka, watadumisha maisha yao wenyewe kwa imani, k.m., kwa kusikia Mungu akinena na kukubalia tunda Lake liwe dhahiri katika maisha yao.

Endelea, chukua jukumu na urudi katika "maisha ya kawaida." Hatua hii itakuongoza kuishi maisha tele kama vile Yesu ameelezea. Na utakapofika Mbinguni utasikia, "Hongera."

**Bwana ni Mchungaji wetu**

Wachungaji huwatunza kondoo wao si kwa sababu wanawapenda jinsi wanavyowapenda wanyama kipenzi kama mbwa au paka, lakini ni kwa sababu kondoo wanawakilisha faida kwao. Ufugaji ni kazi ya mchungaji, biashara yake. Kwa sababu ya mapato ya ziada ambayo yeye hutazamia kupata, anaweza kuwapenda kondoo wake na awatunze kwa upendo. Hata hivyo, siamini wengi wa wachungaji wanaweza kuhatarisha maisha yao mchana na usiku miongoni mwa simba na mbweha kwa sababu ya kuwapenda kondoo kama wanyama kipenzi. Wenye mashamba makubwa katika Uingeleza ya kale waliwapa maskini mashamba yili walime. Lengo lao muhimu lilikuwa ni kupata faida kutokana na mimea. Mapato ya ziada yalikuwa maskini walipata mahali pakuishi na chakula mradi tu waliwatumikia mabwana wao.

***Hivyo ndivyo ilivyo na Bwana wetu Yesu Kristo. Je, Yesu ni mfalme wako?***

Yeye ni Mchungaji wetu ili apate faida kutoka kwa maisha yetu. Faida ni nini? Kutupenda sisi pamoja na wengine ambao atatukuzwa kupitia kwetu. Yohana 15 inasema yakwamba, Yesu hutukuzwa kwa vile tuzaavyo sana. Tunazaa matunda kwa imani katika Mungu na hasa katika Neno lake tunapokuwa marafiki wa karibu naye. Kutukuza kunamaanisha kutoka gizani na kuingia katika nuru, kudhuhirishwa..

Pendo la Yesu kwetu ni zaidi ya vile mawazo ya mwanadamu yanaweza fikiria kama “faida” Yake. Faida yake ni pamoja na uzima wako kwa kuwa wewe ni sehemu ya Biarusi Wake. Hii ni kinyume kabisa na uhusiano kati ya mchungaji wa kawaida na kondoo zake.

Nina shawishika ya kwamba hautaweza kuona miujiza ya kiroho ilioko katika Biblia na katika kitabu hiki, hadi utakapomfanya Yesu kuwa Mfalme wako. Kuna sheria ya kiroho inayowazuia wanaoendelea kuwa “wafalme” wa maisha yao kuona miujiza ya ajabu ya Mungu. Wakati ambao umefika

Reproduction, resale or internet posting prohibited

mwisho wako na huna lingile ila kumfanya Yesu kuwa Mchungaji wako, au kwa maneno mengine, kumfanya Yesu kuwa mfalme wako, basi atakufunulia ukuu Wake, upendo Wake, jinsi anavyokujali, na utashiriki baraka za ajabu maishani!

Tunakuhimiza uweke maneno haya katika mawazo yako unaposoma kitabu hiki, na ujiepushe na "Imani yenye ubinafsi na ya kujifikiria mwenyewe tu," kama vile watu wengine hufundisha. Mimi ni na shauku, na hata zaidi, kuliko baadhi ya walimu wanaofundisha imani isiyo sahihi. Lakini shauku langu linampendeza Mungu na linaeneza makusudi yake wala si kwa sababu ya mapenzi yangu ya ubinafsi kupitia imani.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Sura ya 1
## Maelezo ya Jumla

### Ujumbe Maalum wa Yesu

Ujumbe maalum wa Yesu umetabiriwa katika Isaya 61, na Luka 4 imeandika sehemu ambayo Yesu alitumia kuhubiri kuhusu ujumbe wake maalum "kabla ya Msalaba." Ujumbe maalum wa Yesu ni badilika! Si kubadilika kwa sababu ya kubadikia tu, lakini ni mabariko mema na yenye manufaa, uzima tele alioahidi. Yesu aliahidi kuwahubiri maskini habari njema, uponyaji kwa waliovunjika moyo, kuwaacha huru waliosetwa, na kuwafungulia waliofungwa.

***Kutoka kuwa mfungwa na kuwa kuhani.***

"Roho wa Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao. Kuwaagizia hao waliao katika Sayuni wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe. Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani, watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi. Na wageni watasimama na kulisha makundi yenu, na watu wa kabila nyingine watakuwa wakulima wenu, na watunzaji wa mizabibu yenu. Bali ninyi mtaitwa makuhani wa BWANA; watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wetu; mtakula utajiri wa mataifa na kujisifia utukufu wao" Isaya 61:1-6. Kuna ahadi nyingi za kubadilika katika mistari inayofuata, na kifungu kilicho hapo juu. Soma sura yote.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Je, Yesu anafanya mabadiliko haya vipi, ndani yetu na kwa ajili yetu?**

Kwanza ni lazima ujue huu ni urithi, kitu ambacho tunarithi kutokana na kifo cha mtu aliye mkubwa katika jamii yetu. Tunafaa kuelewa ya kwamba kubadilika kwa ajili ya maisha yetu mema, ni jambo tulioahidiwa na Mungu kupitia kwa Yesu, sio kitu ambacho tunaweza kununua au tunachoweza kufanya kazi ili tukipokeee. Ni kipawa cha bure, na urithi.

"…. urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu" (1 Petro 1:4).

Hata hivyo, kuna masharti katika urithi. Katika utamaduni wa kisasa, utasikia jamii wakisomewa usia. Lazima uwe na imani ili uamini ya kwamba jamaa huyu alikuwachia mali hiyo.

Mungu huweka masharti Yake juu ya urithi Wake ili auhifadhie watu fulani.

***Kuiacha giza  na kupokea msamah wa dhambi.***

"Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kasha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi" (Matendo 26:18).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Kushinda***

"Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu" (Ufunuo 21:7).

***Imani na uvumilivu.***

"Ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu"(Waebrania 6:12).

***Kuishi maisha ya kutubu na kutii***

"husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu." (Wagalatia 5:21)

***Kuwa na macho ya kiroho yaliyofunguka,***

“Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo.” (Waefeso 1:18)

***Anabadilisha faida zetu kwa tumaini na imani na kuchanganyisha na kutii masharti yake.***

Tukisoma Maandiko haya ya Isaya 61 tunapata tumaini. Tumaini ni kama lengo au picha ya kitu kilicho kamilika ya kwamba mambo yatabadilika na kuwa mwema. Hata hivyo tumaini peke yake haiwezi kuleta matokeo. Imani na upendo lazima ziongezwe kwa ahadi.

**Imani ni jambo kubwa kwa Mungu**

“…..kwa maana hakula kwa imani . Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi.”(Warumi 14:23b)

Hi! Huo ni mistari unao washa

“Ni dhahiri ya kwamba hakubna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu mwenyuemwenye haki ataishi kwa imani.”(Wagalatia 3:11)

***Kutoamini ni dhambi***

Hebrews 3:7-12 inasema, “Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, leo , kama mtaisika sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha, siku ya kujaribiwa katika jangwa, hapo baba zenu waliponijaribu, wakanipima, wakaoma matendo yangu miaka arobaini. Kwa hiyo nalichulkizwa na kizazi hiki, nikasema, sikuzote ni watu waliopotoka mioyo hawa; hawakujizuia njia zangu; kama nilivyoapa kwa Hasira yangu, hawataingia rahani mwangu.”

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mungu huongea nasi mambo ambayo aliyemalizisha kabala ya msingi wa ulimwengu hayawekwa na mara nyingi bado hatumaini ingawaji ni mambo yaliyotendwa tayari. Waebrania 4:3 inasema, “maana sisis tulioamini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyosema, kama nilivyoapa kwa Hasira yangu hawataingia rahani mwangu; ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

**Imani ni nini? Inafanya kazi vipi? Tunaipata vipi?**

Wacha tuangalie vile Bibilia inavyosema imani ni inavyofanya kazi na ivle tunavyo ipokea

Tunasikia watu wengi wakisema “imani yako ni gani? Wanauliza kuhusu kuamini kwao kwa kidini ingawaje kuna uhusiano huo sio hali halisi ya imani . wengine husema “ni na imani Mungu atatenda hili ama lile” mara nyingi wanavyo maanisha ni kuwa wanatumaini Mungu atawafanyia jambo, lakini hawana uhakika kamili na hawana msingi wa tegemeo kwa hilo. Hiyo sio imani. Huo ndio wakati wa kutafuta uso wa Mungu ili aongee imani kwako!

***Kuelewa kwa kimawazo kukilinganishwa na kuelewa kwa ufunuo***

Mungu ametupatia jinsia tano ambazo hutupatia ukweli wa ulimwengu wa kwaida tunaoishi.hizi ni kuina, kuguza,kunusa halufu na kuonja. Tunatumia hizi kupata uhakika ya kwamba tuko katika barabar ya usalama tunapoendesah gari, kusikiza wenyewe wakiongea kuhusu mambo na kuendelea. Tunahitaji hizi jinisia ili kuishi katika ulimwengu huu wa kawaida.

Walakini ulimwengu wa kawaida ni matokeo ya ulimwengu usioonekana wa kiroho.Kile tunachoona katika ulimwengu wa kawaida kinaletwa na mwanzo wake ni katika ulimwengu wa kiroho. Mugnu aliwaonya Aadamu na Hawa ya kwamba waishi kulingana na neno la Mungu na watumie jinisia zao tano kwa mambo Fulani. Waligeuzwa na wengi baada yao wamefuta.

reproduction, resale or internet posting prohibited

Waebrania 11:3 inasema, “kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.”

2 Wakorintho 4:18 inasema,“tusivianangalie vinavyoonekana bali visivyoonekana. kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.”

***Imani ni kama hisia ya sita***

Ni njia nyingine ya kupata utadi wa ukweli, njia hakika sana Waebrania 11:1 “Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”

Imani ni kitu , ukweli, kitu ambacho kinaweza guswa au kushikwa, kitu cha kweli kinachoweza kumilikiwa.

***Sasa wacha tulinganishe hisia hizi mbili.***

Ninapogusa meza, ninajua iko. Ni na ushuhuda ya kwamba inaweza kuishikilia sahani ya  ya chakula. Ninapoguzaa ufunuo wa kuelewa Mungu aliponipatia kupitia kwa neno lake na Roho Mtakatifu, pia nimeguza ukweli hakika. Ninajua kile Mungu alichonifunulia katika neno lake kwa Roho Mtakatifu ni hakika, na inaeza kufanya kusudi lile lilifanya itumbue kwangu, walakini hii inadhibitika kama kitu kama ilivyosemwa katika Waebrania 11:1?

***Neno la Mungu wakati limefanywa kwako kupitia Roho Mtakatifu ni mbegu.***

Yesu alifundisha wanafunzi wake kuhusu kanuni hii, hakika aliwaambia katika Marko 4:11 mfano wa mpanzi ulikuwa na maajabu ya ufalme wa Mungu.

Marko 4:3,”Sikilezeni;Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda; ikawa alipokuwa akipanda mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila.”

“Mpanzi huyo hulipanda neno. hawa ndio walio kando ya njia lililopandwa neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao.” Marko 4:14,15

Katika mfano huu neno la Mungu linafananishwa na mbegu ambayo imepandwa katika moyo wa mtu. Hiyo ni kitu! Wakati mkulima anapo pandambegu ya mahindi, hataweza kula mahindi kesho yake, lakini ana kitu katika ardhi na anahakika ya kwamba akiitwaa mbegu , mahindi yake yatakuwa katika mkono wake pale anaweza kutumia na kuila. Wakati Yesu ananpopanda mbegu ndani ya moyo wako kupitia kwa Roho Mtakatifu utajua. Katika Sura sijazo tutachambua hili zaidi.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Chembe hiki cha imani huja vipi?**

***Huja kwa "kumgusa Mungu"***

Warumi 10:17 inasema "imani huja kwa kusikia na kusikia Neno la Mungu." Tazama maelezo ya Kigiriki ya "Neno" Hili neno ni Rhema ambalo linamanisha sauti inayoishi ya mUnug lililoongelewa kwa myo wako kabisa na kupanda kama mbegu.

Bibilia inasema katika Warumi 10:17 "imani huja kwa kusikia (Kile kinachosemwa ) na kile kinachosikia huja kwa kuhubiriwa ( kwa ujumbe unaotoka katika midomo) ya Kristo Mesaya mwenyewe,"

Mtu anaweza kusikiza wahubiri kwa miaka mingi na kusoma Bibilia usiku na mchana na asipojee imanai, mbegu kwa nini?

Hawakupokea rhema kwa sababu Roho Mtakatifu hakuweka nuru lile Neno litoke kwa Logos hadi kwa rhema. Laziam shirikiane na Mungu ili Roho Mtakatifu afanye hili. Ninaelewa ya kwamba hatuko wakamilifu na mtu ambaye hajaokoka anasikia sauti ya Mungu kama hajaokoka hiyo ni neema ya Mungu. Lakini hili linapotokea huyo mtu laziam awe amefungwa moyo wake kwa njia Fulani. Aitha kwa uwaminifu au kwa kulia kwa kufuat msaada.

**Mungu ndiye mwenye mwelekeo wetu wa imani**

Waebrania 11:6 inasema, "lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamaba huwapa dhawabu wale wamtafutao."

Nimeona watu ambao wana imani zaidi kwa kile Mungu anafanya mbegu iliyopandwa ndani ya mioyo yetu huonesha kile Mungu atatundea lazzima tuendelee kumtizamiiia Mungu mwenyewe upendo wake thabihu ya Yesu na mwaminifu wake wa kutenda yaliyo bora kwetu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Neno imani linamaanisha nini?**

Neno imani laitwa "Pistis" (pie-estis) uchambuzi wa kamusi wa Strong's inaelezaaa hivi, "Njia tya kushawishi ya ukweli wa kiungu, ushahidi kwa ujumla ukijimizwa na wazo la uaminifu na kutii kwa utukufu kulipozaliwa na imani. Ni na shawishika ya kwamba na mtawala wa vitu vyote. Ni hakikisho la wokovu ulioletwa kupitia kwa Kristo."

Pili inamaanisha uaminifu na kusimama kwa mtu aliyeona ukweli ambao umeongolewa hapo juu. Mungu hujaribu imani. Yeye huwaamni tu watu waaminifu; watasimama katika uaminifu na kumtii ili aweze kuwategemea.

1 Petro1:6-9 inasema, "mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwakwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwambakujaribiwa kwa imani yenu,ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo naye mwampenda, ijapokuwa hamkumuona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyonenenaka mwisho wa imani yenu, yaani wokovu waroho zenu."

**Maisha ya Abrahimu ni mfano wa imani.**

Ibrahimu aliishi wakti jamii na utamaduni wake wote waliabudu vinyago, vinyago ambavyo mtu angeguza na kuviona. Kulikuwa na kinyago cha kila kitu katika maisha. Siku moja Mungu akanena na Abram,(kabla hajabadilishwa jina) kitu ambacho watu katika siku zake hawakuwa wamesikia.

Mwanzo 12:1-4 inasema, "BWANA akamwambia Abramu, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako,uende mpaka nchinitakayokuonyesha; name nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki na kulikuza jina lako; nawe uwe Baraka. Name nitawabariki wakubarikio naye akulaaniye nitmlaani; na katikawewe jamaa

Reproduction, resale or internet posting prohibited

zote za dunia watabarikiwa. Basi Abramu akaenda, kama BWANA alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani."

***Mungu alisema mambo mengi hapa ambayo yalimtatiza Abramu***

1. Katika siku hizo ni vinyago tu wangelibariki
2. Sarai alikuwa tasa
3. Aliulizwa awache jamii yake ambayo ilikuwa ni kam shirika kubwa. Haukuwa tu utamaduni wake, maisha yake ya urithi wake pia.
4. Abram hakuelezwa aende wapi, lakini alihitaji kusikia sauti ya Mungu ili afike pale alipoahidiwa.

Katika Mwanzo 13 na 14, Abram alipitia majaribu katika Misiri na vita na Chedorlaomer na wafalme wengine ambao walisulubiwa Sodonia na kumchukua Loti, binamu ya Abram, mateka. Baada ya hay Melchizedek alimtokea Abram na kukubali zaka zake. Abram alikuta utajiri mkubwa aliopewa na mfalme wa Sodomu na tamko hili, "Abramu akamwambia mfalme wa Sodomu, nimeinua mkono wangu kwa BWANA,Mungu aliyejuu sana, muumba mbingiu na nchi, ya kuwa sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu wala cho chote kilicho chako, usije ukasema, nimemtajirisha Abramu." (Mwanzo 14:22-23)

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Kisha katika sura ya 15:1 Mungu alimfariji Abram "usiogope Abram mimi ni ngao yako na thawabu yako kubwa sana" hii ilikuwa ni thawabu ya uaminfu na utiifu hata ule wakati Abram hakuwa amesikia Mungu akiongea. Abram alishinda kwa uvumilivu na kutiii ambako Mungu anahitaji kutoka kwetu.

Baadaye katika sura ya 15, Mungu alimuahidi Abram motto ili akiendeleze kizazi chake ambacho kiliahidiwa kuwa kama nyota wa mbinguni. Abram aliuliza jinsi gani atajua hii ni ahadi ya kweli na Mungu akampa agano la damu ambalo

lingeifanya ahadi kutimia. Mwanzo 15:6 inasema, "Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki. "

Kisha baada ya miaka 24 kupita Abram akapata motto na Hagai na mwishowe ahadi yaIsaka ikaja kupita kwa Sara na Ibrahimu. Baada ya matukio mengi katika Mwanzo 16-21. Hatimaye miaka mingi baada ya Isajka kuzaliwa Ibrahimu aliambiwa amtoe kama dhabihu. Tunajua hiyo hadithi ilivyomalizika. Kondoo alitokea katika Mlima Moriah. Imani ya Ibrahimu mwishowe alizawadwia kwa ukamilifu lakini hata hivyo kama Bibilia inavyosema katika Waebrania 11:39-40, "Na watu hao waote wakisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao,hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."

**Hatimaye Mungu alitupatia ushuhuda wa imani ya Ibrahimu uwe mfano kwetu**.

Warumi 4:1-25

Reproduction, resale or internet posting prohibited

*1. "Basi tusemeje juu ya Ibrahimu baba yetu kwa jinsi ya mwili?*

*2. Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake,analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu.*

*3. Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.*

*4. Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni, bali kuwa ni deni.*

*5. Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki.*

*6. Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu Yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo,*

*7. Heri waliosamehewa makosa yao, na waliositiriwa dhambi zao.*

*8. Heri mtu Yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.*

*9. Basi je! Uheri huo ni kwa hao pia wasiotahiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa? Kwa kuwa twanena ya kwamba kwake Ibrahimi imani yake ilihesabiwa ya kuwa ni haki.*

**Kwa maneno mengine, ni kufuata kwa sheria ya Musa kulikoleta Baraka hizi? Paulo alisema la. Ni imani ambayo ililetwa na Neema.**

*10. Alihesabiwaje basi? Alipokwisha kutahiriwa, au kabla hajatahiriwa? Si baada ya kutahiriwa bali kabla ya kutahiriwa.*

*11. Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri ya ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa; ijapokuwa hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki,*

*12. tena awe baba ya kutahiriwa, kwa wale ambao si waliotahiriwa tu, bali pia wanazifuata nyayo za imani yake baba yetu Ibrahimu aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa.*

*13. Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani.*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

*14. Maana ikiwa wale wa sheria ndio warithi, imani. Maana ikiwa wale wa sheria ndio warithi, imani imekuwa bure, na ahadi imebatilika.*

*15. Kwa sababu sheria ndiyo ifanyayo hasira; maana pasipokuwapo sheria, hapana kosa.*

*16. Kwa hiyo ilitoka katika imani, iwe kwa njia ya imani ya neema, ili kwamba ile ahadi iwe imara kwa wazao wote; si kwa wale wa torati tu, ila na kwa wale wa imani ya Ibrahimu; aliye baba yetu sote;*

*17. (kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba ya amataifa mengi); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako.*

*18. Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataiofa mengi, kama ilivyonenwa, Ndivyo utaavyokuwa uzao wako.*

*19. Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa,( akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara.*

*20. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutoamini bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu,*

*21. Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*

*22. Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki.*

*23. Walakini haikuandikiwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake,*

*24. Bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yey aliyemfufua Yesu Bwanawetu katika wafu;*

*25. Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki."*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Je! Na ukijihimiza ya kwamba kiwango chako cha imanikiko chini?**

Habari njema ni kwamba imani ni tunda la Roho, ni kipawa cha bure kutoka kwa Mungu. Ongea na yee, mguse na utaona imani yako ikija bila ugumu mwingi. Kazi itakuwa ni katika kuongea naye na kuvumilia mpaka mwisho lakini imani sio kazi imani huja.

"kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu." (Waefeso 2:8)

**Sura zinazofuata zitagusia mambo ambayo tunapaswa kuongeza katika imani.**

*Imani hutenda kazi kwa upendo: kustahamili na uvumilivu: Kukimbia mbio: Imani hutenda kwa upendo: Kazi za imani: Kuliongea Neno: Viungo vya Petro kwa imani: Mfano wa Mpanzi: Kusikia Sauti ya Mungu - Mto uanotiririka.*

**Kule kusikoonekana**

Mungu muumbaji, Neno la Munngu, shetani, mapepo, malaika, Roho yako, maneno yako. Laana na Baraka. Maombi

↓

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Kule kunakoonekana**

Mwili, vitu vilivyojengwa, serekali, falme za dunia hii hali za kiuchumii. “mielekeo ya kidunia.”

## Sura ya 2
## Viambato Vya Uvumilivu

Tukilinganisha imani yetu iliyokamilika na mchanganyiko wa chakula ambacho lazima tuongeze viungo vingi, Kiambato cha kwanza kujadili ni uvumilivu.

"Na hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi." (Waebrania 6:15)

**Kwa nini ningojee? Nitawezaje kungojea na kuvumilia?**

Neno uvumilivu katika Kigiriki ni Makrothumeo ambalo humanisha kuteseka na kukimia, subira, kupitia mateso kwa wakati mrefu.

Watu wengi watafinyika mioyo siku za usoni ikiwa hawatachukua kuvumilia huku kwa makini na katika mawazo ya Mungu. Nasema kuna sababu mbili kuu kwa hali hii ya kuvumilia. Moja ni kwa ajili yako kukubadisha wewe. Pili ni kwa sababu yaw engine katika ufalme. Amani ya kwamba waumini wachache wangeshindwa katika hali ya kuvumilia kama wangejua jukumu, jukumu kubwa ambalo Mungu amewaaminia kwa ajili ya mabo ya milele.

Nitawezaje kungoja kwa kutosha wakati ambapo uvumilivu wangu wa kuruth ahadi za Mungu yaonekana kukosekana? Kuteseka bila kulalamika ni sehemu ya tunda la Roho, Wagalatia 5:22, ambayo yamaanisha Yesu aliye ndani yako anao uvumilivu wa kutosha. Hiyo ni neema, ama kipawa ambacho hukufanyia kazi, kipawa cha bure. Unahitaji kuwa tupu ufike mwisho wako mwenyewe, na uwache yeye afanye kazi. Atafanya!

**Mwandishi wa Waebrania anatuonya ya kwamba tukiwa wazembe hatuwezikurithi aahadi ambazo Mungu ametupatia kwa imani.**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Waebrania 6:11-20

*11.“Nasi twataka sana kila mmoja wenu aidhihirishe bidii ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho,*

*12. Ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu.*

*13.Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sabbau alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapa, aliapa kwa nafsi yake,*

*14. Akisema, Hakika yangu kubatriki nitakubariki na kuongeza nitakuongeza.*

*15.Na hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi.*

*16. Maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao; na kwao ukomo wa mashindano yote ya maneno ni kiapo, kwa kuyadhibitisha.*

*17.Katika neno hilo Mungu, akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika,alitia kiapo katikati.*

*18. Ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekayo mbele yetu;*

*19. Tuliyonayo kama nanga ya roho, yenye salama, tyenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia,*

*20.Alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.”*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Nanga ya nafsi imechimbwa kabisa ndani ya uwepo wa Mungu**. Unapoenda mbele ya uwepo wa Mungu, nanaga yako imewekwa imara. Tabia yake na nguvu zake zitakupatia uvumilivu unaokosa. Ikiwa umeipokea imani, ahadi ama hakikisho kwa mguso wa kipekee ama kukutana na Mungu kupitia kwa Neno na Roho Mtakatifu, basi nanga yako imewekwa katika ardhi nzuri ya uwepo waMungu.

Kwa nini Mungu anturuhusu kupitia wakati hu wa uvumilivu ili kupata kile tunahitaji? Tulionywa mara nyingi katika maandiko ya kwamba ni lazima tuteseke na tuvumilie majaribu na kujaribiwa kwa imani. Ningetaka kupeana sababu nne kuu, tatu katika sura hii na ya nne katika sura ijayo, ambazo nimepata katika maandiko na katikamaisha kwa sababu ya nyakati hizi za kuvumilia.

**1. Usikose lolote**

"Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta Zaburi. Zaburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu na watimilifu na watimilifu bila kupungikiwa na neno" (Yakobo 1:2-4). Ungetaka vipi usikose lolote? Weka hilo tumaini na maono katika mawazo na moyo wako unapopitia mateso. Ni lengo kubwa vipi uzima tele!

2. **Tabia: ili tabia ikuzwe kwa ajili ya kazi ya Mungu na utukufu wake.**

Hali ambayo imeandikwa katika Warumi 5 ni kama mfinyanzi anaye tengeneza nyungu ya udongo.

Warumi 5:1-5 inasema, "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na iamni kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika dhiki pia; mkijua kuwa dhiki, akzi yake ni kuleta Zaburi; na kazi ya Zaburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabviti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminiwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi. "

Tuanaambiwa dhiki huleta subira ambayo ni neno kama sawa na kuvumilia . subira huleta tabia amabyo huleta tumaini, na tumaini huweka bila kufa moyo wakati wetu wa kuvumilia

Reproduction, resale or internet posting prohibited

kw sababu kama vile inavyosema sisi ni chombo amabcho Roho Mtakatifu hujaza.

Nyungu ikiwa katika gurudumu la mfinyanzi, ni udongo mwepesi. Maji ikiwejkwa kwa nyungu ikiwa bado haija kauka haiwezi kuyashikilia. Kwa hvyo ni lazima mfinyanzi aipitishie katika moto au aweke kwa tanuu iliyo moto ili kuifanya kamili. Baadaye nyungu inaweza kuwekwa kitu na ishikilie iwe ya thamani kubwa.

Warumi 5:5 inasema sisi ni vyombo vya Roho Mtakatifu. Kwa hivyo ni lazima tupitie mioto ya maisha, tukivumilia ili tuwe vyombo sawa kubeba Roho Mtakatifu kwa kazi ya thamani. Tabia inaumbwa na Mungu anantupatia majaukumu zaidi kwa utukufu wake.

**3. Kupokea wokovu kamili ama kuponywa kwa nafsi zetu.**

Mungu anataka tabia yake ipigwe muhuri juu yetu. Msingi wa Neno tabia katika Kigiriki lamaanisha muhuri au kuchoreka. Dhiki yetu huchora mateso ya mukosi juu yetu.

"Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka."(Mathayo 24:13). Uchambuzi wa Strong's unaelezea kuokoka hivi: kuokoka, weka salama na vyema, okoa kutoka hatarini au uharibifu kutoka kwa majeraha au hatari.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

"Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yo yote. Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke hushima, kama chombo kisicho na nguvu kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe. neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu." (1 Petro 1:6-9)

**Kuokolewa kwa nafsi- Na Watchman Nee**[1]

*Kutoka kuokoka kwa nafsi ni tofauti kabisa na kile tunachojua kama kuokoka roho. Roho huokolewa kwa njia ya imani; tukiamini imewekwa milele. Nafsi huokolewa kwa kufuata haya: ni jambo la maisha yetu yote, mwendo wa kumalizwa. Roho huokolewa kwa sababu Kristo ametoa maisha yake kwa ajili yangu; nafsi huokolewa kwa sababu najinyima na kumfuata Bwana.*

*Nafsi ndiyo kiti cha hisia zetu za kimwili. Hatuwezi kuhisi na kufurahia. Tamanio ya maisha haya ya nafsi yanadai kutosheleshwa. Lakini watu wakitafuta kutosheleshwa kwa mambo haya katika maisha haya, watapoteza kutoshelezwa katika maisha yajayo. Yeyote afurahiaye nafsi yake katika maisha haya tayari amepata raha inayoweza kupatikana katika mwili wake; kwa hivyo atapoteza raha hizi katika maisha yajayo. (angalia Mathayo 16:25-26)*

*Yeye ashindaye dhambi huingia mbinguni, hii ni kusamehewa Yule anaye shainda ulimwengu huingia kwa ufalme, hi ni zawadi.*

*Bwana hutufundisha kujiweka kando na dunia. Yeye hutaka kutushawishi tusisikue mateka na vitu vya dunia hii. Kama tukianza kujilinganisha kwa vitu hivi kupita kiasi basi tumeenda kombo. Iwe ni nafasi, chakula, majengo hatutafuti kutoshereka kwetu wenyewe.*

*Mungu huweka chaguo la mbinguni au Jehanamu mbele ya mwenye dhambi. Na vivyo hivyo huweka mbele ya muumini wake chaguo la ulimwengu ama ufalme wake.*

*Kupokea wokovu wa roho ni mwanzo wa imani yetu na kupokea wokovu wa nafsi ni mwisho wa imani yetu.(1 Petro 1:9)*

*Mungu anaonyesha kupitia kwa Kristo ya kwamba ni yeye pekee yake anayeweza kuishi katika kiwango kile alichoweka.*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

[1] Nee, Watchman. Kimetungwa na Sentinel Kulp. Secrets to Spiritual Power. Whitaker House. New Kensington PA. 1998, ukurasa 159-160.

*Kwa hivyo Mungu hakumchagua Kristo afe Kalivari kwa ajili yetu tu, lakini pia awe maisha yetu leo.*

*Wokovu wa Mungu humfanya Bwana Yesu aishi ndani yetu na vivyo hivyo afe kwa ajili yetu Kalivari. Hulipa deni zetu za dhambi zoe, lakini pia huishi ndani yetu ili tusiingie katika dhambi tena. Kama umepata nusu ya wokovu huu pekee yake, bila shaka utakuwa huna furaha na utakaso kuhisi furaha kamili ya wokovu.*

*Hakika Mungu anakuuliza ufanye jambo moja tu: jipeane kwake kwanzia sasa na kuendelea. Inaweza kusemwa hivui kwa neno moja: Jisalimishe.*

*Kile kitu cha kindani sana katika mazingara yetu ni hisia zetu. Kama utaweza kushinda hisia zako, utakuwa mshindi juu ya mazingira mengine yote. Yeyote ambaye hawezi kushinda mazingira hawezi kushinda hisia. Yule amabye ameshinda hisia zake mwenyewe.*

## 4. Kujipatia ufalme wa Mungu kwa vita

“Nikatazamana pembe iyo hoyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme.” (Danieli 7:21,22)

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mara nyingi tunaona nyakati hizi za majaribu na kuvumilia na kuteswa kujaribiwa kwa imani ni kuhisi sisi tu. Ni kweli kuna ukweli katika hili, lakini si ukweli kabisa. Kuvumilia kwingine ni kwa ajili ya kazi Mungu ametenda ndani yetu, na nyingine ni kuhusiana na ufalme wa Mungu na Kanisa.

Umeshtuka! Kuvumilia ni kubwa kuliko unavyo fikiria, kuna thawabu zaidi. Inahusu kutawala pamoja naye. Hili nitaliongole a zaidi katika mlango unalofuata wenye kichwa, “kukimbia mbio.”somo lijalo litaongea kuhusu zawadi na taji. Tunagundua ya kuwa kuvumilia kwetu, mbio yetu ni zaidi yetu tu na inabeba majukumu kuliko tulivyo thania kwanza, nguvu za kuvumilia zitakuja kwa urahisi.

"Kama tukistahimili, tutamiliki pamoja naye; kama tukimkana yeye, yey naye atatukana sisis."(2 Timotheo 2:12)

**Wacha Historia iwe mwalimu wako.**

Ukiangaliaulimwengu utaona ya kwamba watu wote walio faulu katika jambo lolote walikuwa wa manufaa kwa jami na ufalme wa Mungu, walikuwa na jambo moja la kawaida nalo nikuwa waaminifu. Wanasubiri. Miaka mingi iliyopita nilisoma kitabu xcha mtu aliyejitolea maisha yake kuhusu watu waliokuwa maarufu sana katika miaka ya karibu. Alipata kitu kimoja kwa wote ya kwamba walifanikiwa muda mfupi baada ya kushindwa au baada ya kuonekana kama wameshindwa.

Hali na ulimwengu wa kishetani utajaribu siku zote kuvunja moyo na kukushawishi uwache kuvumilai. Kumbuka hili: ukiwa na Mungu, kama hatakufa moyo, utashinda!

Ajabu inafunuliwa katika somo lifuatalo. Ni juu ya kukimbia mbio.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

# Sura ya 3
# Kupiga Mbio
Mambo Zaidi Kuhusu Uvumilivu

Katika sura ya 2 tulizungumza kuhusu haja ya kuvumilia kama kiambato muhimu cha imani. Sura hii inaendelea kuweka mkazo haja ya uvumilivu. Mwaandishi wa kitabu cha Waebrania anatoa onyo kali ya kwamba:

*1. Tuko mbioni, mbio ambayo inahitaji uvumilivu mwingi.*

*2. Tutakuwa katika shida tukivujika moyo na tuondoke kabla ya kumaliza*

*3. Tutapokea tuzo kubwa iewapo tutamaliza mbio.kwa maneno mengine, "kukua au kufa"*

Waebrania sura ya 6 inazungumza juu ya kuondoka kwenye kanuni za

kawaida za Kristo na kuingia katika barabara ya kuridhi ahadi katika imani nauvumilivu. Pia sura hii inasema ya kwamba iwapo hatutavumilia tutaangukana tumuaibishe Mwana wa Mungu. Ingawa siwezi kuelezea mambo yote yalikowuwa katika mawazo ya mwaandishi, mambo haya sio ya mzaha!

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Waebrania sura ya 12 inaelezea onyo hii katika njia inayoeleweka vyem**a!

"Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidinamna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa Zaburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu;ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahilimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kiume wa kiti cha enzi cha Mungu."

"Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo.

Asiwepo mwasherati wala asiyemcha Mungu, kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa(maana hakuona nafasi ya kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi." (Waebrania12:15-17)

***Ninahisi ya kwamba sababu ambayo ilimfanya Esau kutajwa hapa maisha yetu pia.***

Uridhi wa Esau ulikuwa njiani,. Uridhi wetu pia uko njiani. Kama vile

imetajwa katika sura ya 1 na ya 2 ya kitabu hiki, sisi huridhi uzima tele wa Mungu kwa imani na kupitia ahadi Zake ambazo huota kama mbegu ndani ya mioyo yetu. Tahadhari ni ya kuwa kuna wakati wa majaribu na wakati mwingine wa mateso katikati ya kupanda mbegu na kuzaa matunda. Kipindi hiki kinajulikana kama "Kupiga Mbio." Tamaa ya mwili ya Esau ilimwambia, "Nani anayejali ahadi na uridhi wako, mwili wangu unahitaji kula, sasa hivi!" Tusipojihadhari tunaweza kujipata tukimwambia Mungu, "Nimechoka na mateso, nimechoka kungojea, siwezi kuvumilia tena, na nimechoka kabia! Imani kama hii haifanyi kazi." Kuvunjika moyo ni kama vile Esau alichukua sahani ya chakula, ambayo iliushibisha mwili wake ulio mchoyo."

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Pia ni muhimu kujua ya kwamba Esau hakupata aina ya chakula alichokuwa ameomba. Alikuwa ameomba apewe chakula chekundu, nyama nyekundu. Lakini Yakobo alimdanganya na akampa mkate na chakula cha ndengu. Esau hakupoteza haki yake ya mzaliwa wa kwanza tu, bali tama yake ya mwili haikutosheleshwa.

"Esau akamwambia Yakobo, Tafadhali, ulinipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi. Kwa hiyo walimwita jina lake Edomu."

"Esau akasema, Tazama, mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi?"

"Yakobo akampa Esau mkate na chakula cha ndengu, naye akala, akanywa, kisha akaondoka, akaenda zake. Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza." (Mwanzo 25:30,32,34).

***Onyo.***

Esau hangetubu baada ya tukio hili, na sisi pia tunaonywa ya kwamba tabia kama hii inamfanya mtu kuwa na uchungu moyoni.

Pia tunaonywa tuweke tumaini letu katika neema ya Mungu wala sivyo tutajipata wenye uchungu.

Biblia inasema katika Waebrania 12:12-15,

*"Kwa hiyo inyosheni mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza,*

*13. mkaifanyie miguu yenu njia za kunyoka, ili kitu kilicho kiwete kisipotoshwe, bali afadhali kiponywe.*

*14 Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu,ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao;*

*15.Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; Shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo."*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Tunapopiga mbio hii kuna wakati ambao mikono na magoti yetu ya kiroho haina nguvu na hulegea. Tunahisi kuchoka na kuzimia mioyoni mwetu. Kifungu hiki kinatuambia tunastahili kufanya jambo. Kazi yetu ni "kutengeneza njia ambayo ni thabiti, laini na iliyonyooka" ili miguu namikono yetu ya kiroho isije ikapooza, lakini ipate uponaji.

***Kwa nini wakati mwingine tunahisi miguu na mikono yetu ya kiroho iko karibu kuvunjika?*** Haya ni marudia ya Bwana. Tazama mistari iliyotangulia maonyo kuhusu viungo vyetu vya kiroho katika Waebrania 12.

"Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu za mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi?"(Waebrania 12:9). Mungu anajaribu kutuweka katika barabara ambayo itatuwezesha kupokea baraka zake.

***Tunaweza kutengeneza barabara iliyolaini na tuweze kupokea neema ya Mungu kulingana na maagizo yafuatayo ya Biblia:***

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu." (Zaburi119:105).

"Kwa kuwa Wewe Bwana ndiwe kimbilio langu; Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako. Mabaya hayatakupata wewe, wala tauni haitakaribia hema yako. Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe." (Zaburi 91:10-12).

Tukikaa ndani ya Neno la Mungu kupitia Roho Mtakatifu kutafanya njia zetu kuwa laini. Biblia katika Mithali 3:5-6 inasema ya kwamba, tukimtumaini Bwana kwa moyo wote, naye atanyoosha mapito yetu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Sababu za watu kukata tamaa ina uhusiano na shida nyingi au raha nyingi.**

***Mfano 1 – Shida nyingi.*** Ninajua mtu mmoja ambaye alikata tama. Alifikira hajakata tamaa kabisa na Mungu, lakini hakuamini imani hufanya kazi. Dhiki na udhia zilitokea na mbegu ikachukuliwa na Shetani kama vile Marko 4:17 inatasema, "Ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; Kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neon mara hujikwaa."

Matokeo yalikuwa ni kwamba alikuwa na baridi kiroho na akawa mbali na Mungu na mambo ya Mungu pamoja na kanisa. Baadaye alioa mtu alye mzuia zaidi katika utembezi wake na Mungu wa kiroho. Baada ya miaka mingi kupita

aligeuka kwa ajabu na akatubu. Mtu huyu atafika Mbinguni lakini maisha yake hapa duniani ni machache

***Mfano 2 – kupenda raha na mambo ya dunia hii.*** Mfano huu ni watu ambao walioana na wakaanza na kumtumikia Mungu. Lakini baadaye mambo ya dunia, raha ya pesa ikawapa kutoshereka kwingi. Walihudhuria kanisa la kipentekoste, lakini nilishuhudia wakikana kazi za Roho Mtakatifu. Waliasi, watenda yaliyo kinyume na watu waliojitolea kwa Mungu, na bila skaka wakarundi nyuma. Tulipotezana lakini nadhani hawaendelei vyema. Katika Luka 17, mstari wa 26, Yesu alionya dhidi ya kuweka fokasi katika mambo kama, ndoa, ulafi na unywaji. Ingawa hakuna ubaya na kushiriki katika mambo haya, kujishughulisha zaidi na mambo haya ni hatari.

"Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neon, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tama za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neon, likawa halizai" (marko 4:18,19).

***Mfano 3 – tunda la uchungu.*** Ninajua kundi la watu 12 hadi 15 ya watu ambao waliharibu kanisa kwa sababu ya mafikira na tabia zao zizizo za uungu. Wakati kanisa lilimualika mchungaji wa dhamana kulifunga kanisa, likaanza kukua. Jambo hili liliwakasilisha kikundi hiki cha watu, ambao bila shika walijawa na uchungu. Walianza kujaraibu kuharibu kanisa tena kwa kusimama kwenye jukwaa kuimba, bila kualikwa. Wangesimama katikati mwa njia baina ya viti bkatika kanisa na hujifanya wanatoa unabii, wakimtatiza mchungaji. Mwishowe kanisa liliwatimua kisheria. Hatimaye, walifika mwisho na wakajiondoa kama Esau, "Walikula bakuli lao ls supui," na wakawa na uchungu..

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Haya, Hebu sasa tutazame Taji.***

Mwandishi wa Waebrania alisema, "Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na yaliyo na wokovu." Waebrania 6:9.

***Kupiga mbio kwa sababu ya kupokea taji.***

"Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika." (1 Wakorintho 9:25).

"Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi. Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako." (Ufunuo 3:10,11).

*Kifungu hiki kilipewa kanisa la Filadfia.* Kanisa hili linasimamia Waumini ambao Kristo aliwapata bila makosa na ambao hawakupata shida kwa sababu ya imani yao kama kanisa la Simirna.Kwa sababu ya kushinda kwao, wao watapokea taji, zawadi, uwezo, wa kufanya mambo kadhaa katika Ufalme wa Mungu. Elewa ya kwamba Yesu aliwaonya ingawa wako na taji, wasipolishika walicho nacho kwa subira, mtu mwingine anaweza kuitwaa taji yao.

**Taji ni zawadi. Taji ni nini?**

Taji huonyesha mamlaka na uaminifu. Tunapokamilisha mbio sisi hupokea mamlaka ya kiroho. Kukamilisha mbio ni njia nyingine ya kusema "kushinda".

***Mamlaka juu ya nini?***

Mfano katika Luka 19 kuhusu tajiri mmoja aliyewapa wafanyi kazi wake kazi na akaondoka kwenda safari na baadaye akarudi kuangalia uaminifu wao unatuonyesha jinsi moyo wa Yesu ulivyo kuhusu jambo hili la kupiga mbio ukiwa na lengo la kupokea taji.

"Basi akasema, Mtu mmoja, kabaila, alisa.ri kwenda nchi ya mbali, ili ajipatie ufalme wa kurudi. Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, Fanyeni biashara hata nitakapokuja" (Luka 19:12,13).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

"Akamwambia, Vema, mtumwa mwema; kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo, uwe na mamlaka juu ya miji kumi." (Luka 19:17).

*Mji ni nini?*

Katika lugha ya Kigriki neno mji linatokana na neno ambalo maana yake ni kuhifadhiwa katika mji uliozaliwa, ambapo ni pahali penye vita, mabishano na matengano. Mji ambao mtu anakaa kabla ya kuzaliwa mara ya pili. Mungu anataka kutuhamisha kutoka mji wetu wa asili hadi katika Mji wa Mungu, Yerusalemu Mpya, katika Ufalme wa Mungu. Anafanya hivyo kwa kufanya mtu mwingine ashinde kwa niamba yetu, kwa kufanya mtu mwingine akimbie kwa niamba yetu ili wapate mamlaka ya kiroho ndiposa sisi tuwe huru. Hii inalingana na Wakolosai 1:24 ambayo inasema "Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena na yatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake."

***Zaidi yetu.***

Tunapaswa kuelewa ya kwamba taji hii ya maana inahusu Ufalme wa Mungu kuliko haja zetu na hisia njema. Faida zake zina uzito mwingi katika mawazo ya Mungu na ufalme na innastahili kutupea hisia kubwa ya kuwa na jukumu la kukamilisha mbio bila kujali vile tunahisi. Kama vile dada mmoja katika Bwana alituambia hivi karibuni, "Faida ni mwakilishi kama vile yaliyo matokeo ya kukata tama."

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Wafilipi 4:1 ulikuwa mji mmoja wa Paulo.***

"Basi, ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu." (Wafilipi 4:1).

***Ingawa mbio inahusu watu wengi, pia inakuhusu zaidi.***

**Kwa vile sasa unaona zawadi, je mbio ni nini?**

Mbio ni sehemu katika maisha yetu ambapo nilazima tuvumilie mateso tukisimama na Neno la Mungu kwa sababu ya kitu ambacho Mungu ametuaminia kupitia Neno Lake.

Mbegu ilipandwa Aliponena, sasa "mbio" ni kipindi ambacho mbegu iatota hadi wakati wa kuzaa matunda. Kukaa ndani ya Bwana wakati huu ndiyo mbio. Kutokufa moyo wakati mawazo yetu yanalia ndiyo mbio. Mbio siyo kukimbia pahali kidogo kwa haraka, wala ni kukimbia muda mrefu polepole.

Bibla katika Waebrania 12:22-24 inasema, "Bali ninyi mmeu.kilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili."

Waebrania 12:22-24 inaonyesha ya kwamba sisi tunazo nguvu kamazawadi kutoka kwa Mungu inayotuwezesha kumaliza mbio.

Tunao ubatizo wa Roho Mtakatifu, Msalaba, Yesu aliye balozi wetu, malaika, na nguvu nyingi zaidi ambazo tumepewa pamoja na ukombozi.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Paulo aliumaliza mwendo.**

"Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda." (2 Timotheo 4:7).

Imenukuliwa kutoka kitabu kiitwacho God Calling[2] "Kumwita Mungu."

*Karibu na Lengo – Februari 13*

*Katika mbio, sio mwanzo wa mwendo unaoumiza, wala sio hatua katika mwendo mrefu. Lakini watati mtu anaona mwisho wa mwendo ndivyo moyo wake na mishipa inampa nguvu ya kumaliza.*

*Anajitihidi zaidi, misuli yake inakujuka zaidi ya vile angewezakuvumilia.*

---

[2] A.J. Rusell God Calling: Barbour and Company, Inc., Uhrichsville, OH., 1989, Ukurasa 43.

*Kwa hivyo, pia goli yako unaiona sasa, unahitaji kunililia nasauti yako ya mwisho. Je, hauwezi kuona kupitia kuvijika kwa mishipa na moyo wako katika siku chache ambazo simepita yakwamba karibu umalize mbio yako. Jipe moyo! Jipe moyo. Sikia sauti Yangu ya kukutia moyo. Kumbuka Mimi niko pamoja nawe, nikikupa nguvu hadi upate ushindi.*

*Kule mbinguni, rekondi za kuhuzunisha za wale ambao hukimbia vizuri sana, wakiwa na ujasiri wa moyo ulionanguvu, lakini mara tu wanapoona goli ya ushindi, wana kufa moyo na kushindwakumaliza mwendo. Jeshi lote la mbinguni hutamani kulia na kusema jinsi mwisho ulikua karibu, lakini waliokatika mbio wanashindwa kumaliza, bila kujua hadi itakapofunuliwa siku ya mwisho, jinsi walivyokuwa karibu kupata ushindi.*

*Kama wangenisikiliza kwa utulivu jinsi ninyi wawili mlivyokutana na Mimi, Wangejua. Lazima kuwe na masikio inayosikia, vile vile na sauti nyororo.*

**Florence Chadwick.**

Ninakumbuka siku moja nilivyokuwa nikitazama runinga mnamo 1952 na nikashuhudia mwogeleaji hodari Florence Chadwick alipojaribu kuvuja rekondi ya kuogelea katika Catalina, California ya kusini.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Kutoka Wikipedia, encyclopedia ya bure (http://en.wikipedia.org/wiki/Florence_Chadwick)**

*Mnamo 1952, Florence alikuwa mwanamke wa kwanza kujaribukuogelea ubali wa maili 26 kati ya Kisiwa cha Catalina na pwani la California. Alipoanza safari yake ya kihistoria, alizidikishwa na mashua ndogo zilizotazama nyangumi na walikuwa tayari kumsaidia ingawa angeumia ua kuchoka. Saa baada ya lisaaFlorence aliogelea,lakini baada ya masaa 15, hali ya hewa ikawa baya zaidi. Florence akaanza kuwa na wasi wasi na akaambia mamake, ambaye alikuya katika mashua moja, ya kwamba hakuona kama*

*atamaliza safari yake. Akaogelea kwa lisaa lingine moja kabla ya kuomba msaadaavutwe kutoka ndani ya maji. Alipoketi ndani ya mashua Florence aligundua ya kwamba alikuwa amebakiza ubali wa maili moja ku.ka katika Pwani ya California, mwisho wa safari yake. Florence alieleza kwa haraka ya kwamba aliondoka kwa sababu hakuwa akiona mwisho wa safari yake- hali ya anga ilikuwa baya sana nahakuona vizuri. Hangeweza kuona goli yake.*

*Baada ya miezi miwili, Florence aliingia ndani ya maji tena ili ajaribu kuogelea mara ingine. Wakati huu ulikuwa tofauti. Aliogelea moja kwa moja kutoka kisiwa cha Catalina hadi kwenye pwani ya California. Hali ya anga ilikuwa baya kama vile ilivyokuwa maraya kwanza, lakini Florence alifaulu kwa sababu alisema, alipokuwa akiogelea, alikuwa na picha ya pwani ya California katika mawazo yake. Hakupoteza picha ya mwisho wa safari yake kwa sababu alikuwa na wazo kuhusu pwani hiyo katika mawazo yake, na kwa njia hii, akaweza ku.kia lengo lake.*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Sura ya 4
## Kiambato cha Upendo
Upendo wa Damu

Wakristo wengi ulimwenguni hukubali ya kuwa wamevunja mioyo katika safari yao ya imani. Wanasema, “haya mambo ya imani hayafanyi kazi” na hata wale wapikaji nje ya ukristo wa na haraka kuonyesha kushindwa kwa imani.

**Mwandishi Dallas Willard alisema katika kitabu chake, <u>“The Great ommission”</u> [3] (Muamsho mkubwa)**

> *Kuna tofauti kubwa kati ya upande mmoja, tummaini la uzima ndani ya Yesu, inayopatikana ya ukweli katika Bibilia na katika mifano mingi kutoka kwa wafuasi wake, na upande siku, maisha ya undani na uwepo wa kijamii ya wengi wa wale wanao kili kunifuati.*
>
> *Swali lazima litoke: mbona tofauti hii kubwa? Je unaletwa na kitu kilichoko katika utu wa Yesu na kile alichofundisha na kuletea binadamu? Au ni matekeo ya mambo inayojishikilia kwa mashirika ya kikristo na watu wanaposafiri safarini? Je tuko katika wakati ambapo wakristo wengi na uongozi wao kwa sababu fulani, wanakosa mwelekeo mkuu.*
>
> *Ukiona jirani yako na shida na gari unafikiria alipata mikebe.(gari mbaya) na unaweza kuwa sawa. Lakini ukigundua anaongeza maji kidogo kwa Petroli mara kwa mara, hautalaumu gari au wenye kuliunda. Linapokwama au kuguruma na kuzima. Utasema ya kwamba gari halikwenda katika hali zile mwenyewe ameliweka. Na utamshauri awe akaweka mafuta yaliyo sawa peke*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

[3] Willard, Dallas, The Great Ommission, Harper Collins, New York, NY, 2006

*yake katika tanki. Baada ya kazi ya ukarabati labda gari litaenda sawa sawa.*

Kitabu hiki cha imani kinatakja kuzungumza jambo hili na kurahisisha viungo sawa ili imani yako iwe ya hakika, iwe na nguvu na ifanye kazi na kuonyesha matokeo ndani ya maisha yako, na kwa wale ambao wanakutazamia na katika ufalme wa Mungu. Twahitaji tuongeze viungo vya sawa katika safari yetu ya imani. Hii kwa vyovyote vile haiondoi ukuu wa Mungu katika maisha yetu. Mbali inafaa kutuweka kwa njia yake na maisha aliyo twandalia ya utele.

**Petro amenakili viungo vingi muhimu kama imani.**

Tutazungumzia kuhusu viungo hivi na zingine katika kitabu hiki ililiyo pandwa mioyoni mwetu. Huo ndio mwanzo wa imani.******

2 Petro 1:2-11,

*1. Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.*

*2. Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

*3. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tama.*

*4. Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu,katika imani yenu tieni na wema na katika wema wenu maarifa.*

*5. na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu Zaburi na katika Zaburi yenu utauwa,*

*6. na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, upendo.*

*7. maana mambo hayo yakiwa kwenu na kuja tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.*

*8. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake zamani.*

*9. kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenuna uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe.*

*10. maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.*

**Tazama mistari iliyo hapo juu.**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

1. Mungu hutupa sis yote tunahitaji katika maisha na uungu kwa kumjua Yeye.
2. Ahadi zake mingi na za dhamana ni vyombo vya yote tunayohitaji. kama nilivyosema katika sura ya 1, sisi hupokea ahadi zake tunapokuwa na uhusiano wake wa ndanikatika hali ya mbegu ambayo imepandwa katika mioyo yetu. huo ni mwanzo wa imani.
3. Petro anatupatia viungo vingi vin  avyohitajika kuongezwa kwa hali hii ya imani.

**Sura hii inaongea kuhusu Kiambato cha upendo**

"Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo" Wagalatia 5:6.

Kama Mungu amenena na umesikia sauti yake, basi ahadi za Mungu ziko moyoni mwangu, mbegu imepandwa. Lakini

mbegu itafanya kazi ndani ya "moyo safi ardhi nzuri" Nzuri ni nini? Upendo ndio ardhi ambayo itaruhusu mbegu kumea.

> *1 Wakorintho 13:1-9a,*
> *"Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu. pendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu; upendo hautabakari; haujivuni,haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu bali,bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote. Upendo haupungui neno wakati wo wote….*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Imani itafanya kazi tu katika watu ambao wataruhusu Yesu kuishi maisha ya upendo wake kupitia kwao.**

Katika Marko 4, katika mfano wa mpanzi Yesu ananonyeshana ya kuwa kazi kubwa ya shetani ni kuiba neno la Mungu, mbegu ambayo yeye Yesu, amepanda moyoni mwako. Shetanianaweza kuiba mbegu, neno, ahadi ya Mungu kwa njia chache ambazo Yesu anaelezea katika mfano ule. Njia hizi zinatokana na "ardhi", au tabia ya mtu ambaye mbegu imepandwa ndani yake. Hawa ni watu amabo mioyo yao ni watu ambao mioyo yao ni migumu ama hawezi kustahimili majaribu na dhiki au wale wanaotafuta roho za ulimwengu. Kwa upande mzuri nasema "udongo mzuri" au ardhi ambayo mbegu itazaa matunda, ni yule mtu ambaye anaishi maisha na tabia ya upendo, au tabia ya Yesu. Hakika viungo vingine vyote ambao tunazo na tutaziangazia ziko chini

ya sehemu ya upendo kwa sababu ni utu ya Yesu, ambaye jina lake ni upendo.

Ni kweli hakuna hata mmoj wetu aliye mwema kama Yesu: walakini tukiruhusu Neno la Mungu lituhukumu dhaambi zetu, kitu cha ajabu kitatendeka tunapo kiri na kutubu. Tunaoshwa na kuwekwa kwa hali moja na Yesu kama kwamba hatukutenda dhambi kamwe.

Shetani hawezi kupata chochote kwa mtu kama huyo.

**Kutoka The Joyful Heart, Daily Meditation na Watchman Nee. Machi 4**[4]

> *Mtawala wa dunia hii anakuja nahana kitu kwangu. "Mimi sitasema nanyi mneno mengi tena, kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu."(Yohana 14:30)*
>
> *Wakati mwanadamu alijaribiwa na akaanguka Mungu alimlaani majaribu "juu ya tumbo lako utatambaa" Akasema "na mavumbi utakula" basi mahali palipopewa shetani ni dunia, na chakula chake ni kutoka kwa kiel kitu kilichotumiwa kuumba mwanadamu baada ya kugeuka kutoka kwa Mungu. Alikuwa amejipatia "haki za usikwota" katika uumbaji wa kale.*
>
> *Bwana asifiwe kupitia kwa, Kristo shetani hana uwezo juu yetu. Mungu mkombozi alikabiliana na hali kwa kuondoa uumbaji wa kale pale kanisani na kuuleta kupitia Kristo umbaji mpya. Kwa hiyo Mugnu na mtu, hata alipokuwa hapa duniani akadhibitisha ya kwamba mtawala wa ulimwengu huu hakuwa na kitu juu yake kamwe. Na huyu mtu amekalia kiti cah enzi, akidhibitisha ya kuwa shetani hana kitu ndani yetu kw akuwa tumekombolewa. Mwana wa Aadamu*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

[4] Nee Watchman... The joyful heart , Daily Meditations. Tyndale House Publishers. Whearon.cl 19978 Machi 4th ukurasa.

*alitukuzwa ili sisi , wana wengi, pia tukaletwe katika utukufu.*

**Habari njema! Upendo ni tunda. Kama upendo ni tunda lililowekwa ndani yetu basi hiyo ni neema.**

"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria." (Wagalatia 5:22,23)

**ONYO! Tunalo chaguo. Jukumu letu ni nini?**

Waefeso 3:16-19 inasema kama tumepandwa ndani ya upendo basi tunaweza hisi upendo wake wa hakika kando na kuujua kwa akili. Tunaweza kutoa upendo kwa Mungu na wengine baada ya kukutana na upendo wake. Ni hali ya kuendelea. Tunapoona upendo wa Mungu na kujibu kwake na kwa wengine na huo huo upendo tunakuwa imara.

Waefeso 3:17-19, "Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu."

Richard Wurmbrand, mwanzilishi wa "Sauti ya Wateswa" (The voice of the Martyrs) alisema neno upendo huherufiwa kama (s-a-c-r-i-f-i-c-e) kwa Kiingereza.

Kama upendo Yesu anaishi ndani, yetu na ni yeye nditolea. Imani yetu anayeishi maisha ya upendo, basi jukumu letu ni kuchukua msalaba wetu. Inaitwa kujitolea. Inaitwa "upendo ulio na damu."

**Hofu na upendo zinauhusiano**

1 Yohana 4:18 inasema upendo halisi huondoa , hufukuza hofu yote. Tutapataje upendo unaofukuza hofu yote na kufanya imani kufanya kazi? Kujitolea. Penda mtu ambaye hapendeki. Hiyo "itakupanda" katika upendo.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Soma (1 Yohana 4:7-18)**

*7. Wapenzi, nampendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu.*

*8. Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni pendo.*

***9.** Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye.*

***Mstari wa 9 na kumi unasema alitupanda kupitia kwa msalaba wake.***

*10. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisihivi, imetupasa na sisi kupendana.*

*11. Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupas na sisi kupendana.*

*12. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote. Tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu, kwa kuwa tunakaa ndani yetu.*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

*13. Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.*

*14. Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu.*

*15. Kila akiriaye ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu.*

*16. Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye ktika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na*

*Mungu hukaa ndani yake.*

*17. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu.*

*18. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili haitupa nje hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.*

**Unataka upendo wako ulainishwe? Tafuat mtu asiyependeza umpende, na utazame hofu ikitoka kwa maisha na imani ikiinuka.**

Upendo na hofu haziwezi kuishi pamaja. Dawa yangu kwa hofu imekuwa ni kujisongeza kwa uwepo wa Mungu na kumruhusu afanye imani kuinuka. Hii ikifanyika hofu haiwezi kupenda wengine au wewe mwenyewe wakati hofu inakutesa.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Kiu ya Mungu kwa ajili ya umoja na John Walker.**[5]

*"Mkinipenda mtatii amri zangu"(Yohana 14:15)*

*Yesu anapoongea kuhusu upendo hawachi nafasi ya misisimiko au hisia za muda. Unaona upendo kupitia kwa macho ya Baba, na kutoka kwa nafasi hii anaelewa kwa undani ya kuwa upendo wa kweli, wa milele, na wakiungu unaujasiri na nguvu na bado wa uchungu mchafu na wakujitolea.*

*Jiachilia Upendo wa uweza na mkuu aina hii unaweza kuwa na mizizi katika mchanga wa kujiachilia. Tunaachilai haki zetu, mawazo yetu na mipango yetu. Ni huku kujiachilia kwa kabisa kwa Mungu bila kujichunga na kufanya kile Baba alimwambia tu. 1 Yohana 14:10,*

---

[5] ©2008 Purpose Driven Life. Haki zote za kumiliki zimehifadhiwa. Mchungaji Jon Walker ni mwandishi wa www.GraceCreates.com.

*“” Ni huku kujiachilia kwa hakika kuliko mwongozo hadi kwa msalaba.*

*Kama tutafanyika kama Kristo ni lazima tuambatane na mawazo na mipango ya Mungu karibu sana mpaka tuonekane kuwa “mmoja” na yeye kama watu wawili waliooana wanavyo jiachilia mtu kwa mwengine na kuonekana kuishi kama mmoja. Kwa kujiachilia tunatembea kwa karibu sana na Mungu mpaka watu wanapotuona, wananona Baba akifanya kazi.*

*Yesu anafundisha kujiachilia huku anaposema “mkinipenda mtafuata amri zangu.” kwa neno lingine, hakuamrishi uwe mtiivu. Upendo wako kwake utakusukuma kukumbatia makusudi yake.*

*Njia ya Yesu ni kwamba utii amri Mungu kwa sababu ni lazima umtii Mungu kwa kufuata makusudi ya Mungu una mwabudu Muumbaji.*

*Hii pia inakupatia mtazamo wa Kristo kwa mwelekeo wa maisha yako ya kila siku, na kuifanya kila kauli iwe ni wakati wa kumwabudu Mungu. Unapo muacha mtu mwengine achukue nafasi ya kuegeza gari, wakati unapo timiza ahadi ina gharama kuliko ulivyo thania wakati unapo onyesha ukalimu kwa jirani yako ambaye hapendi-Hizi ni nyakati za ibada kwa Mungu kwa sababu unachagua kuwa mtiifu kwa makusudi yake, kando na kutenda mambo kwa njia yako mwenyewe. Na hata kuchgua kutotenda dhambi inafanyika ibada, kwa maana inakuleta karibu na amri za Mungu.*

*Hii inamaana nini? Unapo kabiliana na kukata kauli leo,uliza Mungu akuonyeshe ni njia gani itakuwa ni hali ya kuabudu yeye. Kisha (najua hii ni rahisi kusema kuliko kutend) inawekuwa anakuambia uende.*

*Unapo chukua hatua hii weka macho yako kwa neema na owepo wa Mungu wakati huo. Fanya hili kwa siku yote akuweke nakala ili uweke mwelekeo wako wa kuwa mmoja Mungu na makusudi yake.*

Reproduction, resale or Internet posting prohibited

**Ishi kwa njia hii na uone tunda likichipuka ndani yako na kukuzunguka kama maisha ya utele!**

"Akamwambi, mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako " Mathayo 22:37-39.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Sura ya 5
## Kiambato cha Matendo
Matendo ya aina gani?

**Paulo alisema hatuokolewi kwa matendo.**

Nataka kujifunza neno hili moja kwenu. Je! Mlipokea Roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? Wagalatia 3:2

***Yakobo alisema iamni bila matendo imekufa***

Yakobo 2:17-20 inasema Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake. Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo. Nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema.Mashetani nao waamini na kutetemeka.Lakini wataka kujua,wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai.

***Ukweli wa Mungu ni upi?***

Watu wanakosea kwa upande wa kitako na kungojea Mungu. Wengine hukose kwa upande wa wa kujua mambo katika mikono yao wenyewe.

Watu wa tabaka na nchi zote wanazo. Vita hivi vya kujua na kufanya, haswa katika hali ya wakristo. Kujua ikielezwa kiroho ni uhusiano wa karibu Mungu au mumeo/mkeo kufanya inamaanisha kitendo. Jamii zingine hukosea katika hali ya uhusiano , kujua ila wengine hukosea katika hali kufanya. Wakristo wengi wmechanganyikiwa. Jibu liko katika kile ninaita matendo ya imani, kunywa na matendo ya mwili"

***Bibilia inatueleza tuwe "watendaji wa neno" lakini inatuonya pia ni unahitaji "kujua" kabla ya kuwa watendaji.***

"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana,atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni;Wataniambia siku ile;Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?Ndipo nitawaambia dhahiri

Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu,ninyi mtendao maovu." (Mathayo 7:21-23)

"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliye jenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyuma ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Nakila asikiaye maneno yangu asiyafanye atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga;mvua ikanyesha mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyuma ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa." (Mathayo 7:24-27)

Tazama katika hadithi ya kwkanza hapo juu Yesu hakuheshimu matendo ya "walio tenda" bila ya "kumjua." alisema wataharibiwa.

Katika hadithi ya pili, anaonya wajuaji ikiwa hawakufundisha kujua kwao na kutenda ya kuwa wataharibiwa.

**Mariamu na Martha.**

"Naye alikuwa na umbu lake aitwaye Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake. Lakini Martha alikuwa akihangtaika kwa utumishi mwingi; akamwendea, akasema, Bwana huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie. Bwana akamjibu akamwambia, Martha Martha, unasumbuka na kufadhaika  kwa anjili ya vitu vingi; kinachotaakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema , ambalo hataondolewa." (Luka10:39-42

Hapa katika hadithi hii ya Mariamu na Martha na amini Yesu hakuwa akikataa ya kutimilika na kutenda kazi ya Martha, lakini alikuwa akionesha ya kuwa kabla ya kufanya matendo ya dhamana, uwe na uhusiano wa karibu na yeye.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Kwa nini?***

`Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema.” (Wafilipi 2:13)

Unapo tumia wakati kumjua Yesu katika hali ya kutafakari juu yake. Neno lake, ushirika na Roho Mtakatifu kujiweka katika nafasi ya kumsikiza basi ana”simamia “kutenda” kwako. Ni yeye ndani yako anayetenda matendo ya imani. Jukumu yako ni kusikia na kuitii. Hapa basi Mungu atafanya kazi ya kushirikiana nawe. Vile ni naweza kuwaelezea ni wewe ni “chombo” na Mungu ni “mkono” ndani ya chombo” ni nani anayefanya kazi? Ni Mungu au ni wewe? Jibu ni “ndio.”

**wakamilifu na watu wanao sukumua kutenda wana wakati mgumu kuonyesha majukumu yao.**

***Katika ufalme wa Mungu uhusiano ndio kitu cha mwanzo.***

Mawaitha yangu kwako ni mbadilika! Hata kama ina uchungu vipi. Rafiki yangu mmoja alisema “wakati uchungu” unaopitia unapita uchungu wa kubadilika, basi utabadilika. Kwa mwongozo kwa tabia za kumjua unaweza kwenda kwa tofuti yetu ya mto unatiririka http://www.isob-bibilia.org/flowingriver.htm

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Ninaweza kueleza kazi za imani katika makundi mawili makuu. Kuongea neno na kutii sauti yake.**

***1. Kitu kimoja muhimu katika kazi ya imani ni kunena neno.***

“Lakini yanenaje?Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako yaani ni lile neno la imani tulihubirilo Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maanaq kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata

wokovu." (Warumi 10:8-10) Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani, kama ilvyo andikwa, Naliamini nakwa sababu hiyo nalinena  sisi nasi twaamini na kwa sababu hiyo twanena.

2 Wakorintho 4:13 inasema nitatoa sura nzima kwa ajili ya hii baadaye katiak kitabu hiki.

Kwa ufupi kuongea neno:

(a) Inaumiza mawazo yako na kuweka laini.

(b) Inatukuza shetani

(c) Inaleta malaika pahali ulipo

(d) Humwagilia maji mbegu iliyopandwa katika moyo wako.

(e) Inafurahisha Mungu anaposikia imani yako.

***2. Matendo pia yafuatane na kutii sauti yake.***

Kwa nini Mungu anaweka mkazo juu ya kazi yetu, na wakati mwingine anaonekana kutia mkazo ya kuwa kazi yake ndio mambo muhimu? Ninasema nguvu sana katika uhusiano wetu na Mungu ambao hujuliwa msamaha.

***Kutii kwetu kwa sauti yake kuna nguvu nyingi. Imani kwa sehemu yako. Kumbuka katika sura ya kwanza tulielezea imani:***

***Neno imani lamanisha vipi?***

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Neno la kiyunani la imani ni Pistis(pie- stis). Kwanza inamaanisha kushawishika kwa ukweli katika mambo ya kiungu. Unaposikia neno la Mungu akinena, unasawishika ni kweli, ya kwamba inatoka na shawishi ya kuwa muumbaji ameongea.

Pili, inamaanisha uaminifu na msimamo wa yule aliye tunguka kwa ukweli ulionenwa hapo juu. Mungu hujaribu imani yetu. Anawaamini watu waaminifu, wale kwa kusimama na uaminifu humtii ili awategemee imani ya kweli italeta matendo.

***Kutii***

Kumtii Mungu kuna nguvu Kutii sauti ya Mungu kuna nguvu sana kuliko ni navyo nafasi ya kuchambua katika sura

hii, lakini elewa ndio funguo kwa kukua kwako kiroho, uhusiano wako kwa Yesu na kwako wewe kupokea maisha kwa utele. Ni funguo kwa kuruhusu Mungu akutume kwa kazi yake.

Nimeona wakristo wengi tangu 1979 pia mimi nikiwemo. Nimegundua kwa hali na kwa Neno la Mungu, ya kuwa kutii sauti ya Mungu inaleta tofauti kati ya kushinda na kushindwa. Nimesoma vitabu vingi kutoka kwa waandishi waliohittimu kuniliko mimi ambao wamedhibitisha wazo hili.

Ni muhimu kuwa na kiu kugundua sauti ya Mungu kwako, na pia awe na kiu kujua ni kumtii, gari utakalofanya kila siku, hata kwa mambo madogo maishani mwako. Maisha yaliyojaa hatua ndogo za kutii inaelekezwa kwa maisha ambayo ymebadilika kwa mfano wake na maisha yanayomtukuza. Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba naye atawapa Msaidizi mwingine ili akae nanyi hata milele.

***Yohana 14:15-16 imejaa nguvuza wazo hili.***

Inasema Yesu atadhihirisha, ataionyesha hakika kwa wale wanamsikia na kumtii. Hii ndiyo maana ya kuwa Bwana anapo mfanya Yesu Bwana utaokolewa yaani kukombolewa kutoka kwa hatari na kufanywa mzima. Unapo achilia haki zako za kukata kauli na kuamua kufanya mambo yake Yesu na kukuamuru, basi uhusiano wako na yeye unapanda juu sana. Watu wengi lazima wafike mwisho wao na wajue unyonge wao, na unyonge wa mwenendo wa dunia ili wategemee kabisa kusikia n kutii Munngu. Hili litafanyika kwangu kwa njia kuu sana katika maisha yangu ile niliokoka 1979 kisa kwa njia mpya na kubwa miezi kumi baadaye.

Kutii kwako kuingine kutokana na kushawishiwa na Roho Mtakatifu kwa dhambi zako na sauti nyororo.(wakati mwingi) ili ukiri na utubu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Yohana 14:15-26**

*15. Mkinipenda, mtazishi nit amri zangu*

*16. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;*

*17. ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa hamwona wala hautamtambua; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.*

*18. Si tawaacha ninyi yatima; naja kwenu.*

*19. Bado kitambokidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona. na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.*

*20. Siku ile nanyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, name ndani yenu.*

*21. Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; name nitampenda na kujidhihirisha kwake.*

*22. Yuda (siye Iskariote), akamwambia, Bwana, imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu.*

*23. Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake.*

*24. Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu; nalo neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka.*

*25. Hayo ndiyo niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu.*

*26. Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu ,atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.*

***Ibrahimu alitii sauti ya Mungu na matendo yaliyo kuwa ngumu kwake. Aliambiwa atoe dhabihu, awe mwanawe wa kiume, mwana aliahidiwwa na Mungu. Mungu alimbariki sana kwa kutii kwake.***

Reproduction, resale or internet posting prohibited

"Malaika wa BWANA akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neon hili, wala hukuinizuilia mwanao, mwanao wa pekee, katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzindisha uzao wako kama nyota wa mbinguni, na kama mchanga wa ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao" (Mwanzo 22:15-17).

Miaka iliyopita Ibrahimu na Sara walijaribu matendo lakini hakuleta matunda ya Mungu. Ilikuwa ni wazo lao wenyewe lililozaliwa na akili zao wenyewe bila kusikia sauti y Mungu juu ya jambo hilo. Wakampata mtoto kati ya Ibrahimu na mjakazi wa Sarai, Hagai. Matokeo ni kuwa Ishmaeli alizaliwa. Baadaye Mungu alikubaliana na Sara ya kuwa Ishmaeli atupwe nje, kwa kuwa ndani ya Isaka ndipo agano lilikuwa lipitie.

Mwanzo 21:10-12 inasema,Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu Mfukuze mjakazi huyu na mwanaye maana mwana wa mjakazi hataridhi pamoja na mwanangu, Isaka. Nano hilo lilikuwa baya machoni pa Ibrahimu kwa anjili ya mwanawe. Mungu akamwambia Ibrahimu Neno neno hili lisiwe baya machoni pakom kwa anjili ya huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara sikiza sauti yake kwa maana katika Isaka uzao wake utaitwa.

***Unaweza kumtii Mungu tu kwa kiwango unachoweza kusikia sauti yake.***

Mwanzo utadhania hausikii sauti yake haswa kama "sauti" ya hakika. Inaweza kuwa ni hali ya kusukumwa ndani yako baada ya kusoma neno, jambo Mungu analo kushawishi. Pia inaweza kuwa ni sauti ndani ya Roho na au katika neno kama "Rhema" inayo kusikia kutoka kurasa za Bibilia. Mara nyingi sauti yake inakujia kama picha. Anakupatia pich kwa kuleta matokeo madogo madogo au/na maneno yanayoleta mchoro wa picha. Anaweza leta watu karibu na wewe ambao wana kitu cha kusema au watakukumbusha kichopita. Vile unavyo jikumbusha kusikia sautiyake vivyo hivyo inakuwa wazi

Reproduction, resale or internet posting prohibited

kwako.Unavyoendelea kumsikiza na kumtii ndivyo unakuwa na uweza wa kumsikia na kutii.

**Fanyika mtumwa wa mungu**

Hamjui ya kuwa kwake yye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake Yule mnaye tii kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. (Warumi 6:16)

**Chukua wakati mwingi ukitafakari neno la Mungu.**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Sura ya 6
## Kiambato Cha Kunena Neno

"Likini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani kama ilivyo andikwa, Naliamini nakwa sababu hiyo nalinena sisi nasi twaamini na kwa sababu hiyo twanena" (2 Wakorinitho 4:13).

Roho ya imani hutambulika kama kunena kile mtu ana amini.

**Kwa nini tuongee neno?**

Mungu na mtu wote hutawala kwa maneno. Mungu aliumba kwa maneno yake, na huendelea kuumba na maneno yake walakini hana mamlaka tena kunena maneno yake kwa ulimuengu pasipo kupitia kwa mwanadamu. Mapepo pia ni hivyo hivyo ndiposa wanajaribu kutumia mwnadamu kusema maneno yao. Huu ulimwengu umeumba kutawaliwa na kumilikiwa na maneno.

***Alimpatia Adamu umiliki***

Vinyani mwa watoto wachanga na wanyonyao umeiweka misingi ya nguvu kwa sababu ya wao wanao shindana nawe uwakomeshe adui namjilipiza kisasi; Nikiziangalia mbingu zako na kazi ya vidole vyako mwezi na nyota ulizoziratibisha; Mtu ni kitu gani hata umkumbuke,Na binadamu hata umwangalie?Umefanya mdogo punde kuliko Mungu Umemvika taji ya utukufu na heshima umemtawaza juu ya kazi ya mikono yako Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake. Zaburi (8:2-6)

"Mbingu ni mbingu za BWANA, Bali nchi amempa mwanadamu" Zaburi (115:16)

**Kuangalia mifano ya Mungu akitimis kazi**

Mungu akasema iwe nuru na ikawa nuru;(Mwanzo 1:3)

Mungu akasema, Naliwe anga katikati ya maji likayatenge maji na maji. (Mwanzo 1:6)

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mungu akasema Maji yaliyo chini ya mbingu nay a kusanyike mahali pamoja ili pakavu paonekane ; ikawa hivyo.(Mwanzo 1:9)

Mungu akasema, nchi na itoe majani mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, juu ya nchi; ikawa hivyo (Mwanzo 1:11)

Mungu akasema Naiwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka; (mwanzo 1:14)

Mungu akasema Maji nayajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. (mwanzo 1:20)

Mungu akavibarikia, akisema,Zaeni,mkaongezeke, mkayajaze maji ya baharini,ndege na wazidi katika nchi. (Mwanzo 1:22)

Mungu akasema Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake mnyama wa kufungwa,nacho kitambaacho , na wanyama wamwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo. (Mwanzo 1:24)

Tazama katika haya mandiko hapo juu hakuna kuchojibisana na neno la mungu mbali alikuwa ‘na ikawa hiyo’

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Kisha Mungu akapumzika badaa ya kupatia mwanadamu umiliki.***

Mungu akasema Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu wakatawale samaki wa baharini na ndege waangani na wanyama na nchi yote pia,na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. (Mwanzo 1:26)

Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, zaeni mkaongezeke mkaijaze nchi , na kuiitiisha; mkaitawale samaki wa baharini na ndege wa angaani, na kila kiumbe chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. (Mwanzo 1:28)

Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba Mungu alimaliza kazi akacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. (Mwanzo 2:2)

***Mungu aliongea neno hili kubwa, lililoleta kufufuka kwa Yesu***

Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa. (Zaburi 2:7)

**Shetani huraibu ukweli kwa kuipinda kwa njia mbili-**

Wengine amekosea kwa kunena kwa kusidi wakiamini kunena katika njia ya sawa ni jukumu la mufuasi na wao na si mungu watachagua lakusema na kwa hivyo kile cha kundai na maneno yao. Hii ni hali ya uchawi na ubinafsi. Ndini nyingi za uongo zinaendesha aina hii ya kukili kwa sawa hata kama kukuli sawa ni mbora kuliko kukili kinyumme, sisi kamma wanafunzi lazima tutanue saa yote Yesu kama Bwana kando na matatani na mafamanio yetu

***Tunahitaji kujihathali na mwenendo unaokosa ukweli wa mungu na ina weza mathara katika maisha yetu***

Ukweli ni kuwa Mungu anatamani tushiliki naye na tumuluhusu atupe maneno ya kuongea. Anataka atupatie maneno yake ya imani ili atomize makusudi yake. Katika shamba la edeni Adamu alikuwa ashiliki na neno na mti wa uzima, kila siku na juu ya dunia. Mungu alimpa kutawala, lakini kutawala kwake kulikua kuenezi mapenzi ya mungu peke yake juu na dunia na wanadamu. Adamu akaamua angekuwa na kutawala bila mti wa uzima, na kuwa ageongea neno aliamua lilihitajika kunenwa, mti wa kujua wema na ubaya

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Baada ya Adamu kutenda haya, shetani akaasaa kuwasakili watu kunena maneno yake, na dunia ikajaa kuchanganikiwa. Viumbe vya kiroho vimekuwa vikingangania kutawala maneno ya mwanadamu tangu hapo.

**Uzima na kifo ziko katika nguvu ya ulimi**

Mithari 18:21 inasema Mauti na uzima hua katika uwezo wa ulimi;Na wao waupendao watakula matunda yake.‘’

***Yakobo alielezea hali ya kisayinisi na umuhimu wa kiroho wa maneno***

"Maana twajikwaa sisi sote pia katikka mambo mengi.Mtu asiye jikwaa katika kunena yeye ni mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu. Angalieni twatia lijamu katika vinywa vya farasi ili wamtii hivi twa geuza mwili wao wote.Tena angaliei merikabu ingawa ni kubwa kama  nini na kuchukuliwa na pepo kali zageuzwa na usukani mdogo sana ko kote ana anakoazimia kwenda nahodha.Vivyo hivyo ulimi nao ni Kiambato kidogo nao hujivuna majivuno makuu.Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana.Nao ulimi ni moto ule ulimwengu wa uovu ule ulimi umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi huuwasha moto mfulizo wa maumbile nao huwashwa moto jehanamu. Maana kila aina ya wanyama nay a ndege nay a vitambaavyo  nay a vitu vilivyomo baharini vinafugika navyo vimekwisha kufugwa na waanadamu.Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga ni uovu usiotulia umejaa sumu iletayo mauti.Kwa huo twamhimidi Mungu Baba yetu na kwa huo twalaani wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu.Katika kinywa kile kile hutoka Baraka nalaana.Nndugu zangu haifai mambo hayo kuwa hivyo.JE! chemichemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu?Ndugu zangu Je!Mtini waweza kuzaa zeituni  au mzabibu kuzaa tini?Kadhalika chemichemi haiwezi kutoa maji ya chumvi na maji matamu" (Yak. 3:2-12)

Watalamu wa aliki wameguduwa kuwa sehemu ya kunena katika akili hutawala akili yote. Kwa nini? Mungu alijua alicho kuwa akifanya! Ulimi unabadilisa mwelekeo wa maisha yakekama vile msukani mdogo tu wa meli kubwa unaomua muelekekeo wake

**Mungu alimwambia Joshua kuwa ushindi ungekuja akinena neno tu**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendapo.Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako bali yatafakari maneno yake mchana na usiku upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yalio andikwa humo maana ndipo utakapo ifanikisha njia yako kasha ndipo utakasitawi sana.(Josh. 1:7-8)

**Kuingia kwa pumziko la Mungu.**

***Malaika husikiliza, mapepo yanatoloka***

Yesu ndiye kuhani mkuu juu ya kukili kwetu. Wakati neno la mungu linatangazwa na kuombwa juu ya mtu au hali lina nguvu! Yesu aliumba kila kitu kwa neno lake. Yesu ndiye neno. Yesu alitupatia mamulaka ya kutumia neno kama ni yeye mwenyewe analiongea!

Hapo mwanzo kulikuwako Neno naye Neno alikuwako kwa Mungu naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.Vyote vilifanyika kwa kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Yohana 1:1-3

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Wakati pasaka ilipeanwe kwa isilaeli katika kutoka 12, waisilaile waliambiwa waweke damu ya kandoo asiye na hasia juu ya milango juu na malaika wa kifo (pepo) ‘ akipita juu’ asiwadhuru. Yesu ni mwna kondoo juu ya milango ya wale tunaopenda na tunaombea. Vipi?

Ufunuo 12:11 inasema “Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.”

***Maneno ya vinywa vyetu yatuwasilisha damu***

Ona katika kutoka 12 ya kwamba damu kandoo ilipo kaa katika chombo, haikifanya chochote. Lakini walipochukua na kuipaka kwenye milango yao basi mungu na shetani wangeiona. Majani waliotumia kupaka damu ni majani ya kawaida ambayo hayana dhamana, maneno ya vinywa vyetu hayaonekani ya uzito lakini kukiyotubukisa kwa neno la

mungu ( ambaye ni Yesu mwenyewe) ya kuyutumia kama damu , mungu anaiona na shetani anaina! Yesu anajukua kukili kwetu na kukufanya kwenye nguvu. (wa hibrania 3:1)

Tunapo ongea neno la mugu Yesu ananipelekea baba na kumuhimiza aitimize. (yohana 16:23 ) inasema basi tunaweza kuingia kwenye pumziko na kuacha neno ifanye kazi (Waebrania 4:1) inasema kazi yake ikimalizika kutoka miziki ya ulimwengu kwa hivyo tunaweza kuamini. (waebrania 4:3)

(Waebrania 4:12) malaika hufanya kazi wanapo sikia neno la mungu (Zaburi 103:20) mapepo hutoroka (Zaburi 149:5-9 ) inasema

***Yesu alitupatia mfano***

"Na asubuhi walipokuwa wakipita waliuona ule mtini umenyauka umenyauka toka shinani. Petro akakumbuka habari yake, akamwambia, Rabi, tazama, mtini ulioulaani umenyauka. Yesu akamjibu, akamwambia, Mwaminini Mungu. Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima hu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatuka yake.kwa sababu hiyo nawaambia Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Nanyi, kila msimamampo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hata wasamehe ninyi makosa yenu."(Mak. 11:20-26)

Reproduction, resale or Internet posting prohibited

***Yesu hakusema ni yeye pekee yake angeongea kwa milima.***

Aliwambia wanafunzi wake chochote mnach ouliza mkiomba,amini milima mara nyingi husimamia vizuri katika bibilia. angalia kwa njia Yesu aliongea.

1. kwanza alisema "kwa hivyo na wambia" kama Yesu alitwabia , basin a haki ya kuamini kile alichosem.Yesu aliwambia , yeyote atakayepokea chochote sisi tuko ndani ya mfano wa mungu, na mungu anahitaji tuongee kwa niamba y ake hapa duniani.

2. hakusema useme kile anachotaka kusema. alisema wakati unaomba na kuamini, unapokea yote mambo uliouliza kisha unaweza sema kwa milima, kwa hivyo ni lazima kwanza tushiriki na Yesu katika neno lake kwa roho mtakatifu iili tusike manachotwambia. tunaposikia anochotuambia imani huja kwa kile kinatoka kwetu si tu kile tunacho jitakia.

3. Tunapoelewa tunapaswa kupokea Neno lake, na imani huja kama mbegu mioyoni mwetu, basi lazima tunene hilo neno ambalo tumepokea ili liweze kupita.

Hii sio njia ya kujitisiaya vitu vya kibinafsi. lakini kutusikab sema haya, kunao sheria kuhusu kuongea kwetu ambayo mara nyingi inafanya kazi kwa wasioamini na waaminiokwa usawa. ili sheria hatimaye itafanyikia kila mtu. Tunapokea kile tunachoongea isipokua kile tulichoongea ni katika kutubu dhambi.

4. Katika kifungu kilicho hapo juu, Yesu alitumia neon “sema” mara nne na neon amini mara moja.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Ushuhuda wangu**

mara nyingi tangu niokoke 1979 mungu amenipatia ahadi kwa mahitaji ya dharura. aliniagiza ni mwagiliwe maji ile mbegu kwa kunena ahadi kwa sauti saa zote. kwa wakati mwingine nilinena ahadi kwa zaidi ya miaka mitano kabla ya kuona mlima ukiondolewa. mke wangu na mimi tunanenea maneno mengi ya kibibilia saa zote tunapo omba, tukijumika (Zaburi 91 na Zaburi 23). kuna mengine mentgi. Tuna daftari ya maombi ya kurasa 17 ambao imejaa maandiko ambayo tunajiombea sisi na wengine mara nyingi kila wiki.hii ni kuhusu maadui, Baraka na laana, mambo a kipesa , watoto hudumu na mambo mwengine.

***Onyo , njia ni nyembamba***

katika kifungu kifuatacho cha maandiko, nina amini esu alikuwa akiwafundisha watu jinsi ya kukaa katika ufalme wa mungu hapa duniani. kwa maoni yangu na wahimiza, kuuliza, kutofuta na kubisha, kama njia ya kuomba ili kusimamisha ufalme wake(Mathayo 7:7-12)

Yesu alikuwa akifundisha somo hili hili la ulizo tafuta na bisha katika ( Luka 11) alipokuwa akiwafundisha wanafunzi wake kuhisu maombi . kisha akamalizia fundisho hilo na (Luka 11:13)

tunapo uliza mugu hutupatia ufunuo wa mapenzi yake kwa roho mtakatifu tunapo tafuta mapenzi yake kuhusu jambo hilo. kisha tukipokea mapenzi yake , nia na ahadi yake, tunaweza kuanza kubisha, au kuongea lile neno atakalotupatia (Mathayo 7:13-14)

kuongea nono kikamilifu ni tunda ya uhusiano wa karibu. lakini ninasema ya kuwa Yesu alikuwa akionyesha katika maadiko hapo juu yakwamba kuna hali nyembamba sana kwa kuzaa matunda.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Angalia katika maandiko hapo juu:***

1. njia nyembamba kwa kuona kwangu imeelezewa katika mifano wa " uliza, tatuta na bisha" kumuliza Mungu ni sawa na "kuishi " hii ni katika mazingara ya uhusiano na kumjua.
2. kutafuta ni kugundua mapenzi ya mungu, suluhu ya mungu au mfano/ahadi ya mungu
3. kabisa ni kuwa wakutoacha, na kuongea neno. kuongea neno bila uhusiano wa karibu sio njia nyembamba ya mungu.

Yesu alijua ni watu wachache waliochagua njia ya kuliza, kutafuta na kubisha katika maish. ingewaletea uzima tele.

**Yesu alisitahimili msalaba kwa kunena neno**

Kwa maoni yangu, Yesu alinakili sehemu ya maandiko mengi kutoka (Zaburi 22) au hata yote ambayo iliongewa kuhusu mateso yake msalabani. (Zaburi 22) iliandikwa karne nyinyi kabal Yesu haja zaliwa

Zaburi 22 :31 inasema "Nao watawahubiri watakaozaliwa haki yake, Ya kwamba ndiye aliyeyafanya." Tua kwa muda na usome Zaburi hii yote oune vile Yesu alipitia kusu musalaba.

***Kwa kuto mwanagaza wa maombi una maandiko mengi inaweza kumakiniwa an kuongewa juu ya hali nyingi katika maisha nenda kwa tofauti yetu iliyo hapa chini.***

www.isob-bible.org/abt/prayerbook.ltm

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## Sura ya 7
## Viambato Zaidi Kutoka Kwa Petro

Maagizo haya huonekana kama “mambo ya kale” kwa Wakristo wengi, lakini kuna mengine mengine zaidi ya vile tuonavyo. Kwa hivyo, Wakristo wengi wamo katika “magereza” ambayo hawastahili kuwa. Wamejifananisha kuwa waaminifu kwao wenyewe na kwa Mungu. Wakati mwingine wao huelewa wamejifananisha lakini hawaelewi wamo katika “gereza”. Mara kwa mara adui hufunga milango ya gereza yake kwa undanganyifu wa kuzingatia sheria na desturi za dini. *****

**Makusudi ya Mungu ni kuwa wanadamu waliopotea. Kwa njia gani?**

Tumebarikiwa ili tuwe baraka kwa watu waliopotea na wanaokufa kote ulimwenguni. Mungu alimwambia Ibrahimu, “Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaazote za dunia watabarikiiwa” (Mwanzo 12:3). *****

**Pasipo Utakatifu, hakuna mtu atakaemuona Mungu!**

Namshukuru Mungu kwa vile ametupea haki na utakatifu kama zawadi . Lanini unapoendelea kuzama katika uhusiano wako na anaza kuhisi mabadiliko ya kweli na halisi katika tabia zako za haki na utakatifu. Siongeii kuhusu baadha yake kuwekwa juu yako. Mchezo kama huu wa kidini huzaa watu walio na uchungu na hasira, wakati ambao utakatifu wa kweli huzaa furaha, upendo na matunda yote ya Roho. “Mkavai utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli” (Waefeso 4:24).

***Njia Kuu 35. Njia Kuu ya Utakatifu katika Isaya 35.***

“Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, Njia ya Utakatifu; wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao’ wasafiri, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo” (Isaya 35:8). Isaya 33 inaongea kuhusu hukumu ya Waisraeli kwa sababu ya maisha yao ya dhambi. Isaya 34 inaongea kuhusu Mungu akiwapitisha hatika hali ya kushinda na Isaya 35 inatuonyesha matokeo, ambayo ni utakatifu. Faida zimeandikwa katika sura ya 35. faida hizi ni pamoja na furaha, kusifu, nyikani pamoja na nchi yenye kiu kutabubujika chemichemi ya maji, jangwani kutakuwa na majani, furaha itakuwa kubwa, baada ya kuona utukufu wa Bwana. Inaelezea macho ya vipofu yatafumbuliwa, vilema wataruka-ruka kama kulungu, huzuni itageuka kuwa imani, walio na kiu watapewa maji, na eatu wataishi juu ya adui wao wa kiroho. Utafaidika ukisoma sura hii ukiwa na maoni haya.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Ezekieli 47:1-12 inaonyesha picha ya mto utiririkao.**

Picha aliyoonyeshwa Ezekieli ni ya Hekalu la Mungu na mto unaotoka katika hekalu hilo. Mungu aliongea na Ezekieli na kumwonyesha kwamba huu ulikuwa Mto wa Uzima unaotiririka kutoka kwa Mungu hadi kwenye bahari ya chumvi na kuingia katika maji machafu yaliyooza. Mto huu utayaponya maji hayo na kuyafanya hai. Maandiko katika Ezekieli sura ya 47 yanasema ya kwamba mto ulianza kama kijito kilichotoka chini ya hekalu, lakini mto huu ukaendelea kuwa na maji mengi yaliyotiririka hadi kwenye bahari ya chumvi. Mto huu ulifanya bahari ya chumvi kuwa hai. Kwa kawaida bahari katika Biblia, humaanisha bahari ya wanadamu waliopotea. Mungu alikuwa akimuonyesha Ezekieli kwamba njia pekee ya kuwafanya wanadamu waweze kuishi, ni kwa kuguswa na Mungu, kwa njia ya kitu kinachoitwa Mto unaotiririka kutoka katika uwepo wake mwenyewe.

Katika Yohana 7:38 imeandikwa hivi, "Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, Mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake."

Reproduction, resale or internet posting prohibited




***"Ezekieli Andika"***

Mungu alimwambia Ezekieli katika sura ya 43:10-11 aandike kuhusu picha hii ya hekalu na sheria zake ili watu

wauone na ndiposa waweze kutubu na hatimaye wawe Baraka kwa wengine. Hii ni fundisho ambayo tunapata kwenye picha hii ya mto utiririkao.

Hekalu liko wapi leo? Katika 1 Wakorintho 6: 19-20 tunaambiwa hivi; "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni *Mungu katika miili yenu."*

***Hatuwezi kubarikiwa au kuwa Baraka kwa wengine bila kuwa katika uwepo halisi wa Mungu.***

Tunahitaji uwepo wa Mungu utuweke huru na kutusa.sha, ili tuweze kufanya aina yoyote ya huduma na hata kuomba maombi yaletayo matokeo Hapa kuna utaratibu ambao tunaweza kuufuata ili tuweze kuhisi ujaza wa Mungu katika maisha yetu, kanisa lako na katika uliwengu. "Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali. Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu Mto unatiririka ndani ili kukusa.sha - Mto unatiririka nje ili kuuokoa ulimwengu uliopotea. Mto unatiririka ndani ili kukusa.Mto unatiririka nje ili kuuokoa ulimwengu uliopotea. nyingi na ishara zikafanywa na mitume" (Matendo 2:42-43).

***Tazama mambo matatu ambayo mitume walifanya kila siku ambayo yalisababisha ajabu nyingi na ishara kufanyika:***

*1.* ***Mafundisho ya mitume.*** Hii ni kufundisha neno la Mungu kila siku.


*2.* ***Kuomba****.* Haya yalikuwa aina tofauti za maombi. Kanisa la mwanzo mara kwa mara walikiri wao ni akina nani katika Kristo na walitubu dhambi za watu wote.

*3****. Ushirika na kuumega mkate****.* Walifanya hivyo kila siku ili kuukumbuka mwili wa Kristo na damu ya agano.

******

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Tunahitaji kujua kwamba kuna maadui wanaotaka kumzuia Mungu asionekane kwamba ni kweli yupo pamoja nasi.**




Maadui zetu huja kwetu kwa njia kuu tatu***:***
*Utashi wetu –*
*Akili zetu –*
*Hisia zetu –*
**Hushambuliwa na Mwili, Ulimwengu na Shetani**

Swali:
**Tunawezaje kuwashinda maadui hawa ili tuweze kuingia katika uwepo**
**wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye?**
**Jibu:**
**Mungu ameishatupatia ushindi dhidi ya maadui wote! Njia ya kuingia katika uwepo wake ilipatikana pale msalabani wakati pazia lilipopasuka toka juu hata chini – Marko 15:38. Sasa ni kazi yetu kushirikiana naye. Tunapaswa kubeba msalaba wetu – huo utatupatia ushindi!**

Reproduction, resale or Internet posting prohibited

Katika Luka 9:23-25 Biblia inasema, “Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha. Kwa

kuwa yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza, au kujipoteza mwenyewe?

Neno hilo *nafsi* katika Luka 9 linamaanisha utashi, akili na hisia. Neno kukana linamaanisha kukataa kitu fulani. Ufunguo wa kupata uzima tele na kupokea baraka kutoka kwa Yesu, hii ikiwa ni pamoja na uwepo wake, ni kukamilisha agano la damu kwa kubeba msalaba wetu.

Wengi wetu tunajua kazi nzuri sana, yenye uweza mkuu, iliyohusisha kila kitu, ambayo Yesu aliifanya juu ya msalaba wa Kalivari, jinsi alivyomwaga damu yake kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka katika wafu ili kutupatia uzima. Hatuwezi kuongeza chochote juu ya hayo. Hata hivyo, ili tuweze kunufaika na kazi hiyo, hatuna budi pia kufa. Lazima tubebe msalaba wetu, tujikane wenyewe na kumfuata. Ni lazima tuiangamize nafsi yetu. Uhusiano na USHIRIKA wetu na Mungu umejengwa juu ya msingi wa agano la damu. Kwa wengine jambo hilo linaweza kuonekana geni. Jambo hilo linaweza kulinganishwa vizuri zaidi na ndoa. Watu wengi sana wana ufahamu usio wa kibiblia kuhusu uhusiano huu wa agano la damu. Hebu jiulize swali hili: Je, ungeweza kujadiliana na mchumba wako kuhusu uhusiano mwingine wa kimwili unaoruhusiwa kuwa nao na wanawake wengine baada ya ndoa?

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Agano la damu huchochewa na vifo VIWILI; cha Yesu na chako!**

**Ni kitu gani muhimu sana kuhusu agano la damu?**



Katika 1Petro 1: 18-19 imeandikwa hivi: “Nanyi mfahamu kwamba Katika kitabu cha 1 Petro 1:18-19 tunasoma maneno yafuatayo: “Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu;

bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo." Katika Mambo ya

Walawi 17:11 tunasoma pia maneno yafuatayo: "Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu; name nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi."

**Maisha ya kiroho yanaweza kubadilishana na ile sheria ya mbadala.**

**Agano la damu hubadilisha urithi wa familia yako.**





Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Uridhi wa Jamii.*** Kimsingi, hii ina maana kwamba watu wanaweza kuzaliwa katika familia fulani, na katika familia au ukoo wao huo, wakapokea baraka na laana kama urithi wao. Hata hivyo, baraka na laana zinaweza kubadilishwa. Makabila kadhaa katika bara la Afrika, na pia katika utamaduni wa Wahindi wekundu na katika jamii nyingine za Asia, yamekuwa kila wakati yakitafuta njia  za kubadilishana na watu wengine baraka na laana.

Kabla ya kuumbwa kwa dunia, Mungu alikuwa amepanga kwamba Yesu asulibiwe kulingana na Roho wa UZIMA, na hii ina maana kwamba ile kanuni ya mbadala ilikuwa ikitenda kazi hata kabla mwanadamu hajaumbwa `(Ufunuo 13:8).

Ili agano la damu liweze kweli kufanya kazi, ni lazima kila upande unaohusika umwage damu, au ni lazima viwepo vifo viwili au misalaba miwili. Lazima utu wetu wa kale ufe na kisha tujikabidhi sisi wenyewe na vyote tulivyo navyo kwa Yesu. Jambo la kufurahisha ni kwamba hata Yesu mwenyewe ametoa yote aliyo nayo na kujitoa mwenyewe kwetu!



**Tunapounganisha msalaba wa Yesu na msalaba wetu tunakuwa tumeunganishwa na Mungu. Nguvu hutokea!**

Kila wakati kunakuwa na misalaba miwili inayopaswa kuungana ili kufanya agano la damu.

Hema ni alama yenye nguvu ya misalaba miwili inayofaa kutumiwa kama mwongozo wa maombi. Itatusaidia kubeba msalaba wetu na kutuingiza katika uwepo hasa wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye!


Dondoo kutoka katika kitabu kiitwacho "God's plan and the Overcomers" (Mpango wa Mungu na washindaji), kilichoandikwa na Watchman Nee.

> *"Agano la Kale linatuambia jinsi wateule wa Mungu walivyoishi duniani. Kwanza, Hema lilitumika kama kituo cha makabila 12; baadaye Hekalu ndilo lililokuwa kituo chao. Kituo cha Hekalu kilikuwa Sanduku. Hema, Hekalu na Sanduku ni aina mbalimbali za Kristo. Kadri wana wa Israeli walivyokuwa na uhusiano mzuri na Hema au Hekalu walipata ushindi, na hakuna taifa lililoweza kuwashinda. Ingawa wana wa Israeli walikuwa hawajui kupigana, waliwashinda maadui zao wote waliokuwa wamejifunza jinsi ya kupigana. Lakini wakati walipokuwa na tatizo kuhusiana na*

Reproduction, resale or internet posting prohibited

> *Hema au Hekalu, walichukuliwa utumwani. Haikusaidia kitu kuwa na wafalme wenye nguvu au hekima kubwa, kitu muhimu kilichoangaliwa ni iwapo wamelikosea sanduku la maskani au hekalu. Walipotoa kipaumbele kwa Mungu, ushindi ulikuwa wao. Ndivyo ilivyo hata leo. Tukiuzingatia ushindi wa Kristo, sisi pia tutapata ushindi."*

Unavyoendelea kuwa na ushirika na Mungu, jaribu kujiona kana kwamba unatembea katika Hema kama jinsi makuhani wa Agano la Kale walivyofanya.




Reproduction, resale or internet posting prohibited

Kwanini Hema ni mfano wa maana hivyo katika kurejesha ushirika wa mwanadamu na Mungu?


Angalia, katika mchoro wa 1 Mungu na Adamu walifurahia ushirika na mambo ya ndani kabla ya dhambi kuingia.


Katika mchoro wa 2, baada ya dhambi kuingia, Utukufu wa ushirika ulivunjika, "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23)

Ilihitajika damu ili kurejesha ushirika uliovujika, msamaha wa dhambi zetu. Hii ndiyo gharama ya msamaha.


Ua mbili, Ua wa Nje na wa Patakatifu huashiria Msalaba wa Yesu na msalaba wetu, damu ya pande zote mbili (upande wetu na upande wa Yesu)

*"Nami nitaonana nawe hapo, na kutangamana nawe pale nilipo juu ya kiti cha rehema, katikati ya hayo makerubi mawili yaliyo juu ya sanduku la ushuhuda" (Kutoka 25:22)*




Hema iliongozwa vyumba viwili ili kurejesha Utukufu kupitia damu




Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Sababu ya Mungu kupeana picha ya Hema ilikuwa ni kutumia damu ili kurudisha Utukufu wa ushirika wa kweli.**

## Kwanza: Msalaba Wake



Nyakati za Agano la Kale, kila mwaka Wana wa Israeli walikuwa wakiadhimisha Siku ya Upatanisho ijulikanayo kama “Yom Kippur” Dhambi za wana wa Israeli zilikuwa zikishughulikiwa katika siku hii moja tu ya mwaka, wakati kuhani mkuu alipojiandaa kuingia katika Hema kwa niaba ya wana wa Israeli kwa ajili ya dhambi zao.

Pale kwenye madhabahu ya Shaba, katika ua wa nje, kulikuwa na mbuzi wawili. Mmoja alifungwa kitambaa chekundu shingoni mwake kuonyesha kwamba atachinjwa kwa ajili ya damu. Mwingine alifungwa nje ya lango kuonyesha kwamba angekuwa Azazeli. Mbuzi wa kwanza alichinjwa madhabahuni na damu yake ilipelekwa na kuhani patakatifu pa patakatifu ambapo aliitoa kwa kufukizia kando ya madhabahu ya kufukizia (mahali pa sifa). Uvumba ulipokuwa ukiungua, ulisababisha moshi ujae patakatifu pa patakatifu, na hiyo iliwakilisha (na kuleta hasa) uwepo wa Mungu. Kuhani alinyunyiza damu juu ya Kiti cha rehema mara moja na pia alinyunyiza damu mbele ya Kiti hicho mara saba. Nje ya marago, kila mtu alilala kifudifudi wakati yote hayo yalipokuwa yakiendelea. Hakuna mtu aliyeona chochote kilichokuwa kikifanyika, na hiyo ilimaanisha kwamba dhambi zao zilisamehewa kwa mwaka mzima.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Pili, kuhani aliporudi na kubadili nguo zake, aliweka mikono yake juu ya mbuzi mwingine, Azazeli, kuashiria kwamba dhambi zote zimehamishiwa juu ya kichwa cha mnyama huyo. Kulikuwa na mtu aliyechaguliwa kumpeleka mbuzi huyo jangwani mahali pasipokaliwa na watu na kumwacha sehemu ambayo hawezi tena kurudi au kutoroka. Mtu huyo kwa mfano, alimpeleka mbuzi yule hadi kwenye bonde lililozungukwa na miamba na majabali na kisha mbuzi


yule aliteremshwa chini ili asiweze kutoroka(Mambo ya Walawi 16:21-22).

Sasa kuhani alipoweka mikono yake juu ya mbuzi aliye hai, ili kuanza sehemu ya pili ya ibada, aliungama dhambi zote za wana wa Israeli. Alisema, "Bwana, weka dhambi zangu na za wana wa Israeli juu ya kichwa cha mbuzi huyu. Haya, we mbuzi, ondoka." Mbuzi yule alipokuwa akipelekwa nje ya marago, watu wote walisimama na kushangilia. Watu wote na hata watoto waliweza kuona tukio hilo na kufahamu. Azazeli ni mfano wa Yesu aliye Azazeli wetu, aliyeshushwa chini hata kuzimu kwa ajili yetu huku dhambi zetu zikiwa juu ya kichwa chake. Alichukua dhambi zetu na kuziondoa kabisa, zisionekane tena au kurudi. Zaburi ya 103:12 inasema "Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao." Katika kitabu cha Mika 7:19 tunasoma pia maneno haya "Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zotekatika vilindi vya bahari."

Katika kitabu cha Waebrania 9:12-14 tunapata pia maneno yafuatayo"wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewealiingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kutusa.sha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasa.sha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Pili: Msalaba Wetu**




Yesu aliposema kwamba ni lazima tujikane, tuiangamize nafsi kwa ajili yake, nk., alikuwa na maana kwamba tunapaswa kuikana au kuiambia nafsi “hapana”.

***Nafsi yetu ina sehemu tatu:*** Utashi, Nia (Akili) na Hisia. Patakatifu panawakilisha ile sehemu ya utu wetu, yaani nafsi.Sehemu hiyo ilikuwa na na aina tatu za fanicha au samani zinazowakilisha utashi wetu, Akili na Hisia (Angalia mchoro huo hapo juu). Kwa hiyo tunapoziambia sehemu hizi “hapana” na kusema “ndiyo” kwa yale aliyo nayo Mungu, huku ndiko kuubeba msalaba wetu.

*Utashi wetu -*

*Akili zetu -*

*Hisia zetu* **hushambuliwa - na Mwili, Ulimwengu na Shetani**

**Sasa tutasa.ri hadi kwenye sehemu zote hizo tatu wakati wetu wa maombi na pia tutaendelea na safari na kuwapita maadui zetu hadi katika uwepo wa Mungu!**

Reproduction, resale or internet posting prohibited

## “Mto Utiririkao”
## (Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku)
Kusafiri hadi katika Uwepo wa Mungu

**Maelekezo:**

1. Soma kwanza kurasa 7 za mwanzo, na kisha zisome tena angalau mara moja kwa mwezi. Halafu kila siku, anzia ukurasa huu, na uwe na muda wa kuwasiliana na Mungu angalau kwa dakika ishirini.

2. Utakapoanza na hema ya kukutania, mgongo wako unapaswa kuielekea dunia huku uso wako ukimwelekea Yesu. Hii ni muhimu kwa sababu Roho

Mtakatifu hawezi kukaa na wewe iwapo unaelekea mahali pabaya. (mwelekeo wa kiroho, Matendo ya Mitume 26:18)

3. Nenda hadi kwenye kila “kituo” ushughulike na somo hilo katika hali ya maombi pamoja na Bwana. Tafuta katika Biblia baadhi ya maandiko. Uwe macho kuhusu maeneo yanayohitaji toba, kwa sababu jambo hili ni moja kati ya michango yetu mikubwa, wakati huu tunapokuwa na ushirika na Mungu.

4. Ni vema ukipitia vituo hivi vyote kwa wakati mmoja. Unaweza kufanya hivyo kwa DAKIKA ISHIRINI. Hata hivyo, kama huna muda wa kupitia utaratibu huu wote kwa mkao mmoja, usikate tamaa. Badala yake, anza utaratibu huu asubuhi, na umalize angalau hatua moja. Kisha endelea na hatua ya pili wakati wa chakula cha mchana. Kama unahitaji, endelea siku inayofuata. Hatimaye ishi maisha yanayofuata utaratibu huu na itakuwa kawaida kwako kukaa katika uwepo wake Mungu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Ua wa Nje**

**Kituo cha kwanza: Madhabahu ya Shaba- Msalaba wa Yesu.**

***Madhabahu ya Shaba***

**Msamaha.**

Agano la damu hubadili mabaya yote tuliyo nayo na kuweka mema yote aliyo nayo Mungu. Hata hivyo hatuwezi kupata msamaha wa dhambi bila kumfanyaYesu kuwa Bwana (Warumi 10:9-10).

Anza leo kuwa mkweli mbele za Yesu. Neno la Mungu katika 1 Yohana 1:9 linasema "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusa.sha na udhalimuwote."

Sehemu kubwa ya kubeba msalaba wako ni kuwa KWELI KABISA mbele za Mungu. Unahitaji kuwa wazi kabisa na kumwambia kila kitu. Uwe na muda wa kuumimina moyo wako kwa Mungu kama jinsi ambavyo ungefanya kwa mtu ambaye ni ra.ki yako sana! Biblia inasema katika 1 Yohana 1:7 kwamba "tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusa.sha dhambi yote." Yesu alisema katika Yohana 3:19 kwamba dhambi haina nguvu iwapo watu watakuja kwenye nuru pamoja na kweli, bila kujaribu kuji.cha gizani. Yesu hakufa kwa ajili ya visingizio vyetu. Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu!

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Unahitaji kutembea katika upendo, na ikitokea kwamba umefanya dhambi, kimbilia kwa Mungu, usamehewe.**

"Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti"(Warumi 8:2). Tukimgeukia Mungu kila wakati, na kudumu katika hali ya uaminifu mbele zake, atatushindia makosayetu na vikwazo.
***

**Angalia Mto Utiririkao Kiambatisho cha F ujitathmini mwenyewe kwa uaminifu.**

Kama hakuna dhambi zinazojulikana, basi kiri kwa kinywa chako

maneno yaliyoandikwa katika Wagalatia 2:20 na 2 Wakorintho 5:21.

## Kiambatisho F
## Kujichunguza Kiroho

• **Upendo** - Je unawatendea wengine kwa upendo wa Mungu usio na masharti?

• **Ubinafsi** - Kuweka mahitaji yako mwenyewe juu ya mahitaji ya wengine. Upendo hujishughulisha na ustawi wa mtu mwingine – je wewe unajijali mwenyewe zaidi na kujali tu jinsi unavyojisikia?

• **Kuiba** - Je unaweza kukumbuka fedha ulizopokea kwa mali iliyokuwa si yako?

• **Kulaghai** - Je, ulipata kitu chochote kutoka kwa mtu fulani kwa njia isiyo ya haki?

• **Kusema uongo** - Aina yoyote ya udanganyifu wa kukusudia

• **Kashfa** - Kumsema vibaya mtu fulani. Kumkashifu mtu siyo lazima useme uongo - Je, umewahi kuwasema wengine bila upendo?

• **Ufisadi** - Je, unajisikia hatia kuamsha tamaa usizoweza kuzitimiza kwa haki? Ufasiki, uchafu wote, hata kama ni juu ya mwili wakomwenyewe.

• **Ulevi** - Utumiaji wa madawa ya kulevya, karamu za ulevi.

• **Lugha chafu au matusi** - maneno maovu, mazungumzo mabaya au yasiyo na maana, uchafu, mazungumzo machafu, ya kipumbavu, ya kipuzi, ya upotovu.

• **Wivu** - Kwa kawaida mahali penye mazungumzo yanayohusu makosa au kushindwa kwa wengine, kuna wivu uliojificha.

• **Utovu wa shukrani** - Ni mara ngapi wengine wamekufanyia vitu lakini hukushukuru?

• **Hasira** - Je, umewahi kukasirika?

• **Kulaani** - Umetumia lugha ya matusi.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

• **Utani** - Maneno yasiyohitajika, maongezi ya kipumbavu, kuongea na kutenda kama punguani. Masihara na mzaha na utani wa vitendo unaoelekea kudhoo.sha viwango vitakatifu na vyenye thamani vya maisha. Je, umewahi kulitania kabila fulani au sehemu fulani ya ulimwengu, taifa au mkoa katika nchi yako, au mwanasiasa fulani? Mizaha ya kikabila au kimikoa haina nafasi katika utakatifu.

• **Ukali** - Ulijibu mapigo, ulinung’unika au kurudisha mabaya kwa mabaya?

• **Tabia** - Je, kila wakati una uchu upitao kiasi? Na vipi kuhusu tabia yako ya ulaji?

• **Hali ya kuwa shingo upande** - Unaweza kukumbuka nyakati ambazo kwa makusudi kabisa ulikwepa kufanya wajibu wako kwa ukamilifu?

• **Kizuizi** - Umeharibu imani au matumaini ya wengine kwa kupoteza bure muda wao? Je, umemghilibu mtu aliyekuwa na imani na wewe?

• **Unafiki** - Je, maisha uliyoishi siku za nyuma, yamewafanya baadhi ya watu waone kwamba yale uliyoyasema juu ya Kristo na Injili yake ni ya uongo?

• **Kuvunja nadhiri** - Je, kuna nadhiri yoyote uliyoweka mbele za Mungu ambayo hukuitimiza?

• **Kutokusamehe** - Je, una kinyongo au uchungu dhidi ya mtu mwingine, rafiki au adui?

• **Mafarakano** - Misuguano, roho ya kuwa na vikundi vinavyotofautiana.

• **Kutamani, kuishi kitajiri na kutapanya mali, ula..** Kutumia pesa kupita kiasi kwa kununua vitu madukani. Kupoteza muda bure.

• **Kutowatendea vyema,** au kwa upendo na heshima, wake, waume, watoto na wazazi.

• **Kutoridhika**, kuwa na wivu kwa sababu wengine wana vitu lakini wewe huna.

• **Kuabudu sanamu** - Shauku yoyote katika maisha yako inayozidi shauku ya kuishi na Mungu.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

• **Ugomvi** - Umechochea ugomvi kwa maneno yasiyohitajika?

• **Uchawi** - Kumtawala mwingine kwa hila ili kutimiza haja zako.

• **Kuasi mamlaka** - Mkuu wako wa kazi, mwalimu, mzazi, kiongozi wa kiroho, nk.

• **Kuupenda ulimwengu** - Pamoja na: tamaa za macho - unasoma au kutazama nini? Tamaa za mwili - unatamani nini? Kiburi cha uzima

- Ni jambo gani katika maisha unalo.kiri kwamba unaweza kulifanya

bila Mungu kuhusika? - Kujifanya kuwa mkubwa au mdogo kuliko jinsi ulivyo kwa njia ya mawazo au kwa kuishi.

• **Kiburi** - ni dhambi kubwa kuliko zote. Chunguza maeneo haya.

• Je, unaangalia tu kushindwa au makosa ya wengine au unajishughulisha tu na mahitaji yako ya kiroho?

• Unajihesabia haki na kuwakosoa wengine au una huruma na moyo wa kusamehe, ukitafuta yaliyo bora kwa wengine?

• Je, unawaangalia wengine kwa dharau au unawaheshimu wengine wote na kuwaona bora kuliko wewe?

• Je, unajitegemea na kujitosheleza mwenyewe au unawategemea wengine na kutambua kwamba unawahitaji?

• Ni lazima udumishe hali ya kuwatawala wengine au uko tayari kuacha kutawala?

• Je, ni lazima uthibitishe kwamba uko sahihi, au uko tayari kuiachia haki ya kuwa sahihi?

• Una roho ya kuhitaji tu au roho ya utoaji?

• Unatamani kutumikiwa au una hamasa ya kuwahudumia wengine?

• Unatamani kupandishwa cheo au unafurahi wengine wanapopandishwa cheo?

• Unahitaji kupewa sifa au unafurahi wakati wengine wanapotambuliwa?

Reproduction, resale or internet posting prohibited

• Unasikia kujiamini kwamba unajua mengi, au yale ambayo bado
hujajifunza yanakufanya uwe mnyenyekevu?

• Unajifahamu jinsi ulivyo au hujishughulishi na maisha yako kabisa?

• Unawaepuka watu au unatafuta kuwa karibu na wengine? Uko tayari kuchukua jukumu la kuwapenda watu kwa moyo?

• Unafanya haraka kuwalaumu wengine au uko tayari kukubali
kuwajibika?

• Wewe ni mtu usiyetaka kukaribiwa na wengine au ni mtu rahisi kuwasikia wengine wanapokusihi?

• Wewe ni mtu unayejitetea unapokosolewa au unakubali kukosolewa kwa unyenyekevu na moyo mweupe?

• Unajishughulisha kutafuta kuheshimiwa au kuwa kama ulivyo?

• Unajishughulisha na yale ambayo wengine wanafikiri au yale anayofikiri Mungu?

• Unajitahidi kudumisha hali yako au hadhi uliyo nayo?

• Je, unaona vigumu kuwashirikisha wengine mahitaji yako ya kiroho au uko tayari kuwa wazi?

• Unajaribu ku.cha dhambi zako au uko tayari kuonekana wakati
unapokosea?

• Unajisikia tabu kusema, "Nilikosea, tafadhali nisamehe"?

• Unapoungama dhambi, unaungama kwa ujumla, au unakiri na kuzitaja kabisa dhambi zile ulizotenda?

• Unajutia dhambi zako unapokamatwa au unasikitika kwa kuzitenda na unafanya haraka kutubu?

• Wakati hali ya kutoelewana au migongano inapotokea, unangojea wengine waje kuomba msamaha au wewe ndiye unayeanza kufanya hivyo?

• Je, unajilinganisha na wengine na kujiona kwamba unastahili heshima au je, huwa unajilinganisha na utakatifu wa Mungu na kusikia hitaji kubwa la kupewa rehema?

Reproduction, resale or internet posting prohibited

• Je, una.kiri una mambo machache au huna kabisa mambo ya kutubu au kila siku una moyo wa toba?

• Je, una.kiri kila mtu anahitaji uamsho au kila siku unasikia hitaji la kupata upya ujazo wa Roho Mtakatifu?

• Unajivuna unapokaa na Mkristo mpya au unafurahia ari yake? Uko tayari kujifunza kutoka kwake?

• Je, unaogopa unapokaa na Mkristo aliyekomaa zaidi yako, au una njaa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayotokana na uzoefu wake?

**Upasuaji unahitajika?**

Iwapo Roho Mtakatifu anatuonyesha dhambi, tunahitaji kwenda pale ambapo Bwana alikutana nasi kwa mara ya kwanza. Ni pale msalabani. Tunamuona Yesu akiwa amesulibiwa tena, kwa ajili ya dhambi hiyo, amebeba adhabu yetu.

Damu inachuruzika chini kutoka msalabani. Hali hiyo inapaswa kutushtusha na kutuhuzunisha kwa sababu tunaona hukumu ya Mungu ya kutisha. Tunahitaji kufahamu kwamba ghadhabu yote na hukumu ya Mungu iliwekwa juu ya Yesu msalabani.

Yesu anatusubiri pale, siyo kutuhukumu, bali anafurahi tukienda msalabani na kumpa dhambi zetu. Wakristo wengi wanapotambua dhambi humkimbia Mungu kwa aibu na kujisikia hatia. Dawa ya Mungu ya dhambi ni kwenda Msalabani, kwenda Patakatifu pa Patakatifu katika uwepo wake na kuruhusu tabia yake itawale tabia yako. Utakatifu wake utaondoa dhambi zako. Hii pekee ndiyo dawa. Hatuwezi kufanya jambo hili sisi wenyewe. Ni kanuni ya kuondoa na kuweka. Hatuondoi dhambi zetu, Mungu ndiye anayetujaza utakatifu na upendo wake na dhambi lazima iondoke. Usikate tamaa iwapo inakubidi kufanya hivi mara kwa mara. Mungu hatuhukumu. Anayefanya hivyo ni Shetani. Mungu atakukaribisha kila wakati utakapomwendea. Ukiacha kumwendea hapo ndipo anapohuzunishwa.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

***Tembea katika nuru ya kweli.***

Acha kujidanganya, ikabili dhambi hii kama ilivyo. Iache kabisa kwa moyo wa dhati. Simama upande wa Mungu na kuipinga dhambi hiyo. Kusudia moyoni mwako kutoirudia KAMWE.

**Kuungama:**

“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusa.sha na udhalimu wote.”(1 Yoh 1:9). “BWANA amejaa huruma na neema Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili. Yeye hatateta siku zote, wala hatashika hasira yake milele.Hakututenda sawasawa na hatia zetu, wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu; maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.” (Zaburi 103:8 - 12).

***Msamaha siyo tu kuondoa.***

Msamaha ni neno zito linalomaanisha kukata

na kuondoa kama daktari wa upasuaji anavyokata na kuondoa saratani. Msamaha wa dhambi unamaanisha kwamba dhambi imeondolwa kwako na kuwekwa kwa Yesu aliyeibeba msalabani. Kuungama ni kukubaliana na jinsi Mungu anavyoliona jambo na kulitamka kwa kinywa chako.

Kuungama siyo kutamka tamka tu, ni pamoja na kukubaliana na Neno. Unyenyekevu ni kukubali kwamba umekosea. Je, utafanya hivyo sasa? Uko tayari kama mtoto mdogo kumwendea Baba yako mwenye neema na upendo na kungama dhambi zako na kuomba msamaha kwa unyenyekevu?

“Ee Mungu, unajua upumbavu wangu, wala huku.chwa dhambi yangu… kwa ajili ya jina lako, nisamehe uovu wangu, maana ni mwingi…BWANA kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, ili

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Wewe uogopwe. Ee Mungu Baba yangu, nakuja mbele zako kuungama dhambi yangu (zangu) ya (za): (Sasa zitaje na kuziungama.)

Neno lako linasema kwamba matendo haya au mwenendo huu ni dhambi nami nakubaliana na Neno lako. Sina udhuru. Sitaki tena kufanya dhambi hii ndani ya roho, nafsi na mwili wangu. Nataka kuiacha na kutupa mbali nami. Inanitenganisha mimi na wewe. Inaniharibu. Nataka kuponywa, roho, nafsi na mwili, na pia nataka kuwa karibu na wewe. Napokea msamaha wako. Asante kwa kuweka dhambi hii juu ya Yesu, na asante kwa kuwa aliiweka juu ya Msalaba wake kwa ajili yangu. Najua sistahili msamaha lakini nashukuru kwa kuniweka huru."

Malipizo ni utayari wa kulipa au kurudisha kitu fulani kila inapowezekana. Iwapo sasa umesamehewa mbele za Bwana , uko tayari kumwomba akupe ujasiri wa kuungama na kufanya malipizo kwa wengine uliowakosea? Ukitaka kuwa huru kweli kweli dhamiri yako lazima iwe sa. mbele za Mungu NA wanadamu. Huwezi kumtetea Mungu huku unajiona mchafu mbele za macho ya watu wengine.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Kumbukumbu za kushin wa kwako mbele ya macho yao zitakuingiza ndani sana katika utumwa kila wakati unapowakumbuka. Kama hujawaomba msamaha, hali ya kujihisi una hatia itaiua imani yako na kukuibia mwelekeo na nia yako. Hata hivyo, hupaswi kuungama kila dhambi kwa kila mtu; ni dhambi zile tu ulizowatendea watu unaowajua.

Kanuni: Maungamo yanapaswa kufanywa kulingana na dhambi zilizotendwa. Kama ulitenda dhambi mbele za Mungu peke yake, Mungu atakusamehe na kusahau uliyoyatenda (Zaburi 103:8-13; Isaya 43:25; Yeremia 31:34). Dhambi ulizotenda mbele za Mungu na wanadamu ni lazima uzitubu mbele za wote WAWILI, Mungu na mtu (watu) uliyemkosea (uliowakosea).

Baadhi ya yale yaliyomo katika Kiambatisho F yalichukuliwa kutoka katika vijitabu vya Winkie Pratney vilivyochapishwa katika mtandao wa kompyuta (www)

**Kituo cha Pili: Birika: Neno la Mungu**

*Birika la Shaba*

Kwa kuwa sasa fahamu zetu ziko wazi na tunaweza kuwasiliana na Mungu, hebu twende kwenye Neno.

Neno linasema kwamba kuhani angekufa kama angejaribu kuingia patakatifu kabla ya kusimama

kwenye birika. Hatuwezi kwenda katika uwepo wa Mungu bila kusa.shwa na Neno la Mungu (Waefeso 5:26-27).

Birika litatuondolea uchafu wa dunia. Litakuwa pia kioo cha kutuhukumu, litatuletea katika akili zetu mambo tunayopaswa kurekebisha mbele za Mungu.

Neno litahuisha nafsi zetu ili tuweze ku.kiri kiroho na kuwa kinyume na maneno ya pepo yanayokuja katika akili au fahamu zetu. Neno linatuambia pia kwamba Shetani amekwisha hukumiwa (Yohana

16:11). Hakikisha unasema maneno haya kwa sauti "Shetani umekwisha hukumiwa, umeshindwa!"

Reproduction, resale or Internet posting prohibited

Tumia dakika mimgi katika Neno!

a. Tumia kitabu chako cha sala

b. Tumia kitabu chako cha "ISOB" au kitabu kingine cha kujifunzia Biblia.

c. Soma kitabu cha Mithali

d. Soma Zaburi sura moja au zaidi.

e. Soma vitabu vingine vinavyohusu Biblia au soma tu Biblia na umwombe Roho Mtakatifu akutafsirie. Soma Biblia yote kwa mwaka mmoja.

f. Sikiliza mafundisho au kanda za nyimbo zenye Neno la Mungu.

### Kituo cha Tatu: Pazia la Kwanza:

***Pazia la kwanza: Kushukuru***

**Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu.**

Kwa kuwa sasa umekaa katika Neno, unajua uko sa. mbele za Mungu na kwamba Shetani amehukumiwa, basi unayo mengi ya kumshukuru Mungu! Hata kama huoni kwa haraka mambo ya kumshukuru Mungu jaribu kuyatafuta. Kama umeshindwa kuyapata, mshukuru kwa Neno lake linalosema kwamba unao ushindi ukiendelea kulishikilia Neno. Mshukuru pia Mungu kwa ahadi alizokuahidi ambazo bado hazijatimia katika maisha yako.

### Kituo cha Nne: Utashi wako

***Meza ya Mkate wa Wonyesho***

Kituo kinachofuata kipo ndani ya Patakatifu Hapa ndipo unapompa Yesu utashi au mapenzi yako na Yeye anakuonyesha mapenzi yake, unampa ufahamu wako na Yeye anakupa ufahamu wake, unampa hisia zako na Yeye anakupa hisia zake. Huku ndiko kuubeba msalaba wako, kujikana mwenyewe na kumfuata Yesu (Luka 9:23).

Reproduction, resale or Internet posting prohibited

Badilisha haja za moyo wako (hata kama ni nzuri) kwa ajili ya mpango au mapenzi ya Mungu katika maisha yako. Weka chini matakwa na mipango yako na umwombe Mungu akuonyeshe mapenzi yake na mipango yake kwako. Kila wakati Mungu huangalia utashi au mapenzi yetu; hii ndio maana ya mkate wa wonyesho. Mkate ni unga uliosagwa, ukachanganywa na mafuta na kuokwa motoni. Matakwa yetu na hamu zetu ni lazima kila wakati zitolewe madhabahuni zisagwe na kuchomwa.

Hii ni sadaka maalum kabisa kwa Mungu, kwa kuwa ni utashi wetu, na yeye hawezi kutulazimisha wala kutuamrisha kufanya hivyo. Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu (Warumi 12:1-2).

Amua kusamehe hata kama hujisikii kufanya hivyo. Hii ni nafasi ya kutubu na kuacha njia za kidunia na kuzifuata njia za Mungu. Tunapoacha njia mbaya, tunapata nguvu za Mungu (Mdo 26:18 na 2 Kor 3:16). Badilisha tamaa za mwili, uwe na tunda la Roho. Tunda la Roho ni: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi (Wagalatia 5:19-23).

### Kituo cha tano: Nia yako

*Kinara cha Taa cha Dhahabu*

Badili nia au mawazo yako ya zamani uwe na nia ya Kristo. Katika 2 Kor 10:4-6 tunaambiwa kwamba vita viko katika mawazo na fikra zetu. Na kwamba ngome ni mawazo yetu. Mawazo haya hutufanya tuwe mbali na elimu ya Mungu. Kuna mengi ya kusema hapa kwa sababu mawazo yetu ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Tunapaswa kuyaweka huru mawazo yetu. Kwa njia gani? Tulipokuwa watumwa wa dhambi tulitumia Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ambao ni mawazo yetu. Sasa tunapaswa kutumia Mti wa Uzima ambao ni Neno la Mungu. Siwazi tena na kuamua, bali natumia akili zangu kwa sababu ni makusudi ya Mungu, na hiyo ndiyo kusikia na kutii!  Hii pekee ndiyo itakayoangusha ngome katika akili zetu. Tukiuona utukufu wa Mungu kama Paulo alivyouona alipokuwa njiani kuelekea Dameski, hatuwazi tena, tunasema tu, “Bwana, unahitaji nifanye nini.” Mara kwa mara pepo hutushitaki na kushambulia akili zetu kwa kutumia nusu ukweli. Katika Isaya sura ya 11 tunaambiwa kwamba Mungu hubadilisha maarifa yetu ya asili na kutuwekea yale ya Roho

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mtakatifu, yaani Roho wa Bwana, hekima na ufahamu, shauri na uweza, maarifa na kumcha Bwana.

Tunahitaji mawazo au nia zetu zifanywe upya kwa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu (Warumi 12:2). Wakati mwingine hatujui kuomba jins itupasavyo. Katika Warumi 8:26 tunaambiwa kwamba tukiomba kwa lugha, tutaomba sawa sawa na mapenzi kamili ya Mungu. Kwa hiyo kila unapoomba kwa lugha utakuwa unaomba sawa sawa na Neno la Mungu na pia sawa sawa na mapenzi ya Mungu. Ile sehemu inayohusika na usemi au kunena, hutawala akili, na hivyo nia au mawazo yako hufanywa upya na kusawazishwa ili yaweze kuuambia mwili wako utende mapenzi ya Mungu.

## Kituo za sita: Hisia zako

*Madhabahu ya kufukizia uvumba*

Badilisha hisia zako za zamani zilizosababishwa na mwili wako na ulimwengu, na nafasi yake ichukuliwe na tunda la amani, furaha, upendo, tumaini, nk. Hapa ni mahali pa dhabihu za sifa. Soma Zaburi 145-150 kwa sauti kubwa, kama hujisikii kumsifu Mungu moyoni mwako. Mungu anawatafuta watu wanaomwabudu katika Roho na kweli (Yohana 4:24). Kutoka katika mahali hapa pa sifa, Mungu atakutafuta na atahitaji kuwa pamoja nawe!

Reproduction, resale or internet posting prohibited

Mpatie hizo hisia ambazo umekuwa uki.cha; labda ni machozi yako, labda ni kuinua kwako mikono, au labda ni kumfunulia tu hisia zako za kweli. Songa mbele, hakuna mwingine anayeangalia isipokuwa Yeye!

Mbele ya madhabahu hii kuna pazia linalo.cha au kutenganisha patakatifu pa patakatifu na uwepo wa Mungu. Mungu anataka upite katika pazia hilo mara nyingi zaidi ya vile unavyohitaji. Atakusaidia kufanya hivyo. Hakuna mwanadamu wa kawaida anayeweza kuingia hapo bila kufa. Pazia hili lilipasuka kutoka juu hata chini wakati Yesu alipokufa msalabani, akatuwezesha kuingia katika uwepo wa

Mungu kwa damu yake, na kuonyesha kwamba kifo chake kimeondoa kizuizi kilichosababishwa na dhambi. Kizuizi hicho kilikuwa kinatuzuia kuingia katika uwepo wa Mungu. Msifu Mungu kwa ukweli huu.

Patakatifu pa patakatifu ni mahali aambapo hakuna mwanga au taa isipokuwa kwa ajili ya Mungu. Kuhani Mkuu aliweza tu kuingia hapa mara moja kwa mwaka, tena kwa masharti maalum. Ukweli ni kwamba madhabahu hii iliingia Patakatifu pa Patakatifu pamoja na Kuhani Mkuu mara moja kwa mwaka. Hii inaashiria kwamba kusifu kwako na kuabudu hakuishii hapa bali ni mlango wa kuingia katika uwepo wake, na mambo hayo huenda pamoja nasi.

## Kituo cha saba: Roho Yako - Uwepo wa Mungu

### *Sanduku la Agano*

Sasa Mungu atakuvuta na kukupitisha katika pazia hadi Patakatifu pa Patakatifu - penye uwepo hasa wa Mungu.

Hili hapa Sanduku la Agano. Limefunikwa na Kiti cha rehema kilichonyunyiziwa damu. Tulihitaji rehema kwenye madhababu ya shaba, yaani msalaba, mwanzoni kabisa. Lakini sasa katika uwepo wake kuna ufahamu mkubwa wa rehema yake na damu ya Yesu kwa namna ambayo Roho Mtakatifu pekee ndiye awezaye kukuonyesha. Rehema zake ni za milele. Ni kama haiwezekani kabisa kuandika rehema zake jinsi zilivyo, ni lazima mtu apate uzoefu wa rehema hizo.

Katika kila upande kuna malaika wakubwa wanaolinda kila kitu. Hapa pia hakuna nuru kabisa au taa isipokuwa kwa ajili ya Nuru ya Mungu. Kumbuka, sanduku la agano lipo sasa ndani ya mioyo yetu! Sio tena kitu cha nje. Sisi ni hekalu la Mungu. Tafakari jambo hilo.”Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?” (1 Kor 3:16).

Reproduction, resale or internet posting prohibited

**Yaliyomo katika Sanduku la Agano yanaashiria mambo makubwa matatu:**

***Mana au Neno la Mungu:*** Unapokuwa katika uwepo wa Mungu, Neno la Mungu lililofunuliwa huwa hai! Kama unao muda, hapa ni mahali pazuri sana pa kufungua Biblia yako na kumruhusu Bwana aseme nawe. Matunda yanayohitaji katika maisha yetu hapa ulimwenguni yanapatikana katika Neno la Mungu (2 Petro 2:1-11).

***Mbao za sheria:*** Huu ni ukumbusho wa thamani kwamba sheria ya Mungu imeandikwa katika mioyo yetu. Siyo tena orodha ya mambo tunayopaswa kufanya au kutofanya.

***Fimbo ya Haruni:*** Hii inamaanisha huduma yetu iliyopakwa mafuta ya kuwa watendakazi na mashujaa wa maombi kwa ajili ya Mungu. Kulikuwa na .mbo 12 zilizovunjika za mti wa mlozi zilizowekwa Hekaluni kwa amri ya Mungu. Fimbo mojawapo ambayo ingechipua kimiujiza wakati wa usiku, ingekuwa ile ambayo mmiliki wake ni mhudumu aliyechaguliwa na Mungu. Ni Mungu pekee anayetupatia huduma, na tunatambua ni huduma gani pale tu tunapokuwa katika uwepo wake (Hesabu 17:8).

Hapa ndipo tunapoweza hasa kupokea ahadi za Mungu katika Neno lake. Tunapozipokea hapa, tunajua kwamba tutakuwa nazo! Neno la Mungu katika wa.lipi 4:19 linasema "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Hapa unakuwa katika utukufu! Huu hapa utajiri wote wa mbinguni unakungojea. Anza kumshukuru Mungu kwamba mambo haya matatu siyo tu kwamba yapo mbele zako, bali pia yako NDANI yako. Siyo tu kwamba yako NDANI yako lakini damu na kiti cha rehema na malaika wanakulinda kwa hayo. Katika Zaburi 91 tunasoma kwamba malaika zake watakulinda katika njia zako zote. Sasa umeandaliwa kuwa mwombezi hasa. Unashiriki huduma ya Ukuhani Mkuu wa Yesu na

Reproduction, resale or internet posting prohibited

kuwaombea wengine ipasavyo. Yesu alisema katika Yohana 15:7 “Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.”

**Kubeba msalaba wako huzaa matunda.**

Huu unapaswa kuwa muda mzuri wa kustarehe na kufurahi katika uwepo wa Mungu. Tumia muda wa kutosha hapa katika hali ya ukimya na kufurahia kuwa pamoja naye. Hupaswi hata kuongea. Mungu anafurahia jambo hili. Wewe pia utalifurahia. Jambo hili ndilo lililozungumzwa katika somo hili, yaani kuingia katika uwepo wa Mungu! Usisome tu jambo hili na kuendelea. Amua kabisa kwamba kila siku utafanya zoezi la kuingia katika uwepo a Mungu. Jambo hili ni muhimu sana ili kupata ushindi katika maisha hayana yale yajayo.

**Tumezungumzia mengi yaliyo ya muhimu kuhusu imani. Ningependa kukupatia jambo moja lakuweka maanani katika mawazo yako kuhusu hoja hii.**

***Kusikia Mungu akikunenea binafsi ndio jambo la pekee ambalo litazaa imani na kwa hivyo uwe na maisha tele. Hii huja tu kwa mtu ambaye:***

1. Anaelewa ya kwamba yeye ni mudhaifu bila kuwa na imani ya Mungu.
2. Ana mazoefu ya kuchukua muda na kuweka bidii ili kuwasiliana na mungu kila siku.

Reproduction, resale or internet posting prohibited

---

[i] Wakati neno kamusi limetumiwa, inarejelea kamusi ya Microsoft ambayo imotelewa katika Microsoft Word.